BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2019

# 021 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE

# (CSEE) 2019

# 021 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624, Dar es Salaam
Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI ........ IV
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 2
2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha ........ 11
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ........ 13
2.2.1 Swali la 3: Kuongeza Msamiati wa Kiswahili ........ 13
2.2.2 Swali la 4: Fasihi Simulizi ........ 17
2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno na Mjengo wa Tungo ........ 20
2.2.4 Swali la 6: Maendeleo ya Kiswahili ........ 24
2.2.5 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya ........ 29
2.2.6 Swali la 8: Ufahamu ........ 35
2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ........ 40
2.3.1 Swali la 9: Uandishi ........ 40
2.3.2 Swali la 10: Uhakiki wa Ushairi ........ 47
2.3.3 Swali la 11: Uhakiki wa Riwaya ........ 54
2.3.4 Swali la 12: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 64
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA ........ 70
4.0 HITIMISHO ........ 70
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 72
KIAMBATANISHO A ........ 73

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2019. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, watahiniwa, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya watahiniwa ni ishara inayoonesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kuhusu mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa ufanisi na yale waliyoshindwa kuyapata.

Taarifa hii, imechambua sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kujibu kwa usahihi au kushindwa kujibu maswali hayo kama ilivyotakiwa. Matokeo ya uchambuzi huu yamebainisha baadhi ya sababu zilizochangia watahiniwa kutojibu maswali kwa usahihi kama vile kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo na kukosa maarifa kuhusu kanuni na matumizi ya lugha kwa jumla. Uchambuzi uliofanyika kwa kila swali umebaini pia mambo yaliyosaidia watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa wa mada mbalimbali katika somo, kuzingatia kanuni na matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Sababu za watahiniwa kupata alama za wastani zimebainishwa hususan katika kutoa majibu yasiyojitosheleza.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ili kupata ufumbuzi wa kasoro mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii. Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, watahiniwa wanaohitimu Kidato cha Nne watapata ujuzi katika kujieleza na kufafanua dhana mbalimbali kwa ufasaha.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo Maafisa Mitihani, Walimu na wafanyakazi wa Idara ya Utafiti, Tathmini na Huduma za Kompyuta walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika taarifa hii.

Dr. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2019 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huu ulikuwa na maswali 12 yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C kwa kuzingatia mada za *Ufahamu*, *Matumizi ya Sarufi na Utumizi wa Lugha*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili* pamoja na *Fasihi*. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A, B na maswali matatu (3) kutoka sehemu C.

Mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2019 ulifanywa na watahiniwa **424,843**. Kati ya watahiniwa hao, waliofaulu yaani waliopata daraja A hadi D ni **385,792** sawa na asilimia **91.31** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kiwango hicho cha kufaulu kwa jumla ni cha juu zaidi kwa asilimia **1.99** ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2018 ambapo asilimia ya waliofaulu ilikuwa **89**.**32**.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na yale yaliyojibiwa vibaya katika mtihani huu. Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni *vizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha kufaulu kimeanzia alama **65** hadi **100**, huku kiwango cha wastani kikianzia alama **30** hadi **64** na kiwango hafifu kikianzia alama **0** hadi **29**. Aidha, majedwali yenye takwimu na chati mbalimbali vimewekwa ili kufafanua viwango hivyo vya kufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya **kijani** inawakilisha kiwango kizuri cha kufaulu, rangi ya **njano** inawakilisha kiwango cha wastani na rangi **nyekundu** inawakilisha kiwango hafifu cha kufaulu. Hata hivyo, sampuli za majibu ya watahiniwa kwa kila swali zimeambatanishwa ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huo kwa kuonesha jinsi watahiniwa walivyotoa majibu yaliyokidhi/yasiyokidhi haja za maswali waliyopewa katika mtihani huu.

Kwa jumla, uchambuzi huu utaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuinua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inafafanua uchambuzi wa kina wa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanyika vizuri, wastani na yale yaliyofanyika vibaya. Aidha, sababu za kufaulu kwa watahiniwa kwa kiwango cha juu, wastani au cha chini zimeelezwa bayana kwa kila swali. Sampuli za majibu ya watahiniwa kwa kila swali zimeambatanishwa ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huo.


### 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA

Sehemu A ilikuwa na maswali mawili. Swali la 1 lilikuwa la kuchagua na lilikuwa na vipengele kumi na swali la 2 lilikuwa la kuoanisha lenye vipengele vitano. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua

Swali hili lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kuelewa dhana mbalimbali zinazohusu mada anuai za somo la Kiswahili. Swali lilihusu mada za *Aina za Maneno, Mjengo wa Tungo, Fasihi Simulizi, Fasihi kwa Ujumla na Ngeli za Nomino*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo matano kwa kila kipengele katika vipengele kumi alivyopewa na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 424,128 sawa na asilimia 99.8 ya wote waliofanya mtihani. Swali lilijibiwa vizuri sana ambapo asilimia 85.7 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 1**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 1. Watahiniwa 298,586 (70.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6; watahiniwa 64,892 (15.3%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10 na watahiniwa 60,650 (14.3%) walikuwa na kiwango hafifu kuanzia 0 hadi alama 2.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengi (70.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa walikuwa na uelewa wa dhana zilizotahiniwa kwa baadhi ya vipengele vya swali hili na kushindwa katika vipengele vingine. Asilimia 15.3 ya watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana zilizotahiniwa, hivyo walichagua kwa usahihi herufi yenye jibu sahihi. Aidha, watahiniwa wachache (14.3%) walishindwa kutoa majibu sahihi kwa vipengele vingi na kupata alama hafifu kutokana na kukosa uelewa wa dhana mbalimbali zilizotahiniwa katika swali hili. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa umefafanuliwa katika vipengele mbalimbali vya swali hili kama ifuatavyo:

(i) Neno lipi kati ya maneno haya linaweza kudokeza mtenda au mtendwa?

A Kiunganishi

B Kivumishi

C Kihisishi
D Kiwakilishi
E Kielezi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno katika muundo wa sentensi. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili waliweza kuchagua kwa usahihi herufi D *Kiwakilishi*, neno ambalo hudokeza mtenda au mtendwa wa jambo katika sentensi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa juu ya dhana ya kiwakilishi kuwa ni *neno linalosimama badala ya nomino.*

Aidha, watahiniwa wengine walikosa maarifa ya kutosha kuhusu aina mbalimbali za maneno, hivyo kuchagua vipotoshi *A Kiunganishi*, *B Kivumishi*, *C Kihisishi* na *E Kielezi*. Uteuzi wa kipotoshi *A, Kiunganishi*, unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kutambua kuwa kiunganishi hakidokezi mtenda au mtendwa bali kinaunganisha dhana mbili au zaidi. Uteuzi wa kipotoshi *B, Kivumishi* unatokana na watahiniwa kutokuelewa kuwa kivumishi ni *aina ya neno ambalo hutoa taarifa zaidi juu ya nomino au kiwakilishi*, pia uteuzi wa kipotoshi *C Kihisishi*, unadhihirisha ukosefu wa maarifa juu ya dhana ya kihisishi kuwa ni *neno linaloonesha hisia fulani au mkazo wa jambo lisemwalo*. Vile vile, uteuzi wa kipotoshi *E Kielezi*, unaonesha watahiniwa hawakujua kwamba, kielezi ni *neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu vitenzi*.

(ii) Ni sentensi ipi **haina** kitenzi kisaidizi?
A Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa mtiifu.
B Watoto wanatakiwa kulala mapema ili wawahi shuleni.
C Paka alikuwa anataka kula chakula cha mbwa.
D Juma alikuwa anasoma kitabu cha hadithi za mapenzi.
E Robert Kelly anataka kuja kutumbuiza mwezi Desemba.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mjengo wa Tungo* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua mpangilio wa vitenzi katika tungo. Watahiniwa waliojibu vizuri kipengele hiki waliweza kuchagua kwa usahihi herufi *A Mwalimu Julius*

*Kambarage Nyerere alikuwa mtiifu* kuwa ni sentensi isiyo na kitenzi kisaidizi kutokana na sentensi zilizokuwa katika machaguo mengine kuwa na vitenzi visaidizi. Watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu *aina za vitenzi vya Kiswahili* na mahusiano ya vitenzi katika tungo. Walibaini pia katika sentensi hiyo kuwa neno *alikuwa* lilifanya kazi ya kitenzi kishirikishi kwa kuwa halikuambatana na kitenzi kikuu.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi B, C, D na E kutokana na kukosa weledi kuhusu kazi na mahusiano ya vitenzi katika tungo, hivyo walishindwa kubaini kuwa tungo hizo zilikuwa na vitenzi visaidizi na vitenzi vikuu. Kimsingi, kitenzi kisaidizi huambatana na kitenzi kikuu katika tungo yoyote. Kwa mfano, uteuzi wa kipotoshi *C Paka alikuwa anataka kula chakula cha mbwa*, sentensi hii ina vitenzi visaidizi viwili; *alikuwa* na *anataka* vinavyosaidia kitenzi kikuu *kula* ili kukamilisha dhana ya kutoa taarifa. Uteuzi wa kipotoshi *B Watoto wanatakiwa kulala mapema ili wawahi shuleni* ulikuwa na kitenzi kisaidizi *wanatakiwa* ambacho kimeambatana na kitenzi kikuu *kulala*. Waliochagua kipotoshi *D Juma alikuwa anasoma kitabu cha hadithi za mapenzi* hawakubaini kuwa sentensi hii ilikuwa na kitenzi kisaidizi *alikuwa* kilichoambatana na kitenzi kikuu *anasoma*. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi *E Robert Kelly anataka kuja kutumbuiza mwezi Desemba*; sentensi hii ilikuwa na vitenzi visaidizi viwili ambavyo ni *anataka* na *kuja* vilivyoambatana na kitenzi kikuu *kutumbuiza*. Uteuzi wa kipotoshi E ulitokana na maono ya watahiniwa hao kuwa neno *anataka* na *kuja* kuwa ni kitendo kinachokamilisha sentensi hiyo.

(iii) Ni seti ipi inawakilisha kikamilifu wahusika wa fasihi simulizi?

A Vitu, mahali, wanyama, binadamu, fanani na maleba
B Hadhira, wanyama, maleba, binadamu na fanani
C Hadhira, binadamu, wanyama, vitu, mahali na fanani
D Fanani, vitu, mahali, binadamu, maleba na wanyama
E Wanyama, manju, binadamu, vitu, mahali na maleba

Swali hili linatoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutambua wahusika wa Fasihi Simulizi. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili waliweza kuchagua jibu sahihi *C Hadhira, binadamu, wanyama, vitu, mahali na fanani.* Aidha, wapo watahiniwa waliokosa uelewa kuhusu wahusika wa fasihi simulizi kwa kuchagua vipotoshi A, B, D na E. Uteuzi wa vipotoshi *A Vitu, mahali, wanyama, binadamu, fanani na maleba*; *B Hadhira, wanyama, maleba, binadamu na fanani*; *D Fanani, vitu, mahali, binadamu, maleba na wanyam*a na *E Wanyama, manju, binadamu, vitu, mahali na maleba* walishindwa kutambua kuwa "maleba" ni mavazi yavaliwayo na wahusika kulingana na kazi ya fasihi waitendayo na siyo aina ya wahusika wa fasihi simulizi.

(iv) Bainisha seti ya maneno inayofaa kuingizwa kwenye kamusi kwa kuzingatia mpangilio wa alfabeti.

A Jabali, jadhibika, jabiri, jadi, jalada
B Jabali, jabiri, jadhibika, jadi, jalada
C Jabali, jadi, jadhibika, jalada, jabiri
D Jabiri, jabali, jalada, jadi, jadhibika
E Jabali, jalada, jabiri, jadhibika, jadi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno*, mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa wa kutumia kamusi kwa kuzingatia mpangilio wa alfabeti. Watahiniwa hao walichagua jibu sahihi *B Jabali, jabiri, jadhibika, jadi, jalada* kwani walikuwa na ujuzi wa kupanga maneno katika kamusi kwa kuzingatia alfabeti A – Z. Baadhi ya watahiniwa walichagua vipotoshi A, C, D na E kutokana na kukosa ujuzi wa mpangilio wa alfabeti katika kamusi. Kwa mfano, uteuzi wa kipotoshi *A Jabali, jadhibika, jabiri, jadi na jalada*, walishindwa kutambua kuwa neno *jadhibika* halikutakiwa kuandikwa kabla ya neno *jabiri* kwa kuwa mpangilio wa alfabeti unaonesha herufi "b" katika neno *jabiri* huitangulia herufi "d" katika neno *jadhibika*. Hali kadhalika, uteuzi wa vipotoshi C, D na E ulitokana na watahiniwa kutozingatia mpangilio sahihi wa maneno katika kamusi.

(v) Ni sifa ipi haitofautishi fasihi simulizi na fasihi andishi?

A Ukubwa
B Uhifadhi
C Uwasilishaji
D Ukuaji
E Ueneaji

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua katika kutofautisha sifa za fasihi simulizi na fasihi andishi. Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu sahihi *A Ukubwa* kuwa sio sifa inayotofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi kwani hakuna kifaa au chombo kinachoweza kupima ukubwa wa kazi yoyote ya fasihi. Pia, hakuna kipimo cha ukubwa wa ujazo ambao unatofautisha tanzu hizo kwani zote hubeba maudhui yanayolenga jamii husika. Wapo watahiniwa waliochagua vipotoshi B, C, D na E kutokana na kutoelewa matakwa ya swali. Uteuzi wa vipotoshi *B Uhifadhi, C Uwasilishaji, D Ukuaji* na *E Ueneaji* si sahihi kwani vinadhihirisha sifa anuai zinazotofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi.

(vi) Jozi ipi ina vipengele sahihi vinavyounda umbo la ndani la kazi ya fasihi simulizi?

A Falsafa, muundo, ujumbe, wahusika
B Mandhari, msimamo, ujumbe, dhamira
C Ujumbe, mtazamo, migogoro, dhamira
D Ujumbe, msimamo, dhamira, wahusika
E Lugha, mgogoro, falsafa, mtindo

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu vipengele anuai vinavyounda umbo la ndani (maudhui) la kazi yoyote ya fasihi. Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu sahihi *C Ujumbe, mtazamo, migogoro na dhamira* kwani walikuwa na maarifa ya kutosha katika kutofautisha fani na maudhui katika kazi ya fasihi simulizi. Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, D na E kwa kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu vipengele vya maudhui katika kazi ya fasihi simulizi. Kwa mfano, uteuzi wa kipotoshi *A falsafa, muundo, ujumbe* na *wahusika* unaonesha uwezo mdogo wa

watahiniwa wa kutambua vipengele vya maudhui kwani seti hiyo ilikuwa na vipengele viwili vya fani yaani *muundo* (mpangilio wa visa na matukio) na *wahusika* (watendaji wanaopewa majukumu na msanii). Aidha, uteuzi wa vipotoshi vingine vyenye maumbo ya nje (fani) katika fasihi simulizi kama vile "mandhari" (chaguo B), "lugha" na "mtindo" (chaguo E) vinaonesha wazi kuwa, watahiniwa hao walishindwa kutofautisha vipengele anuai vya fani na maudhui.

(vii) "Ng'ombe zangu wanatoa maziwa mengi" kosa lililojitokeza katika tungo hii ni lipi kati ya haya?

A Unyumbuaji wa maneno
B Udondoshaji wa herufi
C Unyambulishaji wa maneno
D Upatanisho wa kisarufi
E Uongezaji wa kiambishi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ngeli za Nomino* na lilipima ujuzi wa mtahiniwa wa kubaini mpangilio mzuri wa maneno katika tungo. Watahiniwa waliochagua chaguo sahihi *D Upatanisho wa kisarufi* walikuwa mahiri katika mpangilio wa ngeli za nomino na namna zinavyotumika katika sentensi/tungo. Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, C na E kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu ngeli ya kwanza *Yu, A – Wa* katika upatanisho wa kisarufi na hivyo kushindwa kubaini kosa katika tungo "Ng'ombe zangu wanatoa maziwa mengi." Uteuzi wa vipotoshi *A Unyambuaji, C Unyambulishaji* na *E Uongezaji wa kiambishi* ulitokana na watahiniwa kukosa uelewa wa dhana hizo kuwa, zote zinahusu uongezaji wa viambishi katika kiini cha neno ili kupata maneno mapya. Pia uteuzi wa kipotoshi *B Udondoshaji wa herufi* iliyomaanisha kuondoa silabi au herufi bila kuathiri maana ya neno wakati katika tungo "Ng'ombe zangu wanatoa maziwa mengi" hapakuwa na herufi iliyodondoshwa bali ilikuwa na kosa la upatanisho wa kisarufi.

(viii) "Serikali imeweka mikakati kabambe **ili** kupunguza umasikini." Neno "ili" katika sentensi hii ni aina gani ya neno?

A Kielezi
B Kiunganishi
C Kiwakilishi
D Kihisishi
E Kivumishi

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno kama zilivyotumika katika sentensi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *B Kiunganishi* walikuwa na uelewa juu ya aina za maneno hasa dhana ya kiunganishi kuwa ni *maneno yanayounganisha dhana mbili au zaidi,* hivyo wakiona kuwa neno "ili" limeunganisha tungo "Serikali imeweka mikakati kabambe" na "kupunguza umasikini." Watahiniwa wengine walionesha kutokuwa na umahiri kuhusu aina za maneno, hivyo walichagua vipotoshi A, C, D na E. Uteuzi wa vipotoshi ulichangiwa na watahiniwa kutojua maana zilizo katika aina za maneno hayo ambapo *A Kielezi* ni neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu vitenzi, *C Kiwakilishi* ni neno linalosimama badala ya nomino, *D Kihisishi* ni neno linaloonesha hisia fulani kuhusu jambo lisemwalo na *E Kivumishi* ni neno ambalo hutoa taarifa zaidi juu ya nomino au kiwakilishi.

(ix) Mpangilio sahihi wa vipashio vinavyounda lugha ya Kiswahili ni upi?
A Mofimu, kishazi, kirai, neno na sentensi.
B Mofimu, neno, kirai, sentensi na kishazi.
C Neno, kirai, kishazi, sentensi na mofimu.
D Neno, mofimu, kirai, kishazi na sentensi.
E Mofimu, neno, kirai, kishazi na sentensi.

Swali lilitoka katika mada ya *Mjengo wa Tungo* na lililenga kupima uwezo/ujuzi wa mtahiniwa wa kuchambua dhana na lilimtaka mtahiniwa kuonesha mpangilio sahihi wa vipashio vinavyounda lugha ya Kiswahili. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili waliweza kuchagua kwa usahihi herufi *E Mofimu, neno, kirai, kishazi na sentensi*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa kuhusu mjengo wa tungo ambao huanza na kipashio kidogo kwenda kipashio kikubwa zaidi ambapo mofimu ni *kipashio kidogo kabisa cha kimofolojia chenye maana ya kisarufi ambacho*

*hakiwezi kugawanyika*. Mofimu hufuatiwa na *neno* ambalo ni *sehemu ya umbo au tungo inayotokana na sifa au asili ya utendaji kazi katika sentensi*. Neno hufuatiwa na kirai ambacho ni *kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi kisicho na muundo wa kiima na kiarifu*, kikifuatiwa na *kishazi* ambacho ni *tungo yenye kitenzi chenye kutoa taarifa Fulani*. Kipashio cha mwisho (kikubwa zaidi) ni sentensi ambayo ni *tungo yenye neno moja au zaidi ambayo hutoa taarifa kamili yenye muundo wa kiima na kiarifu*. Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A, B, C na D kwa kuwa walikosa maarifa juu ya mpangilio sahihi wa vipashio vinavyounda sentensi za lugha ya Kiswahili.

(x) Ni jambo gani linalodhihirisha upekee wa kazi fulani ya kifasihi?
   A Muundo wa kazi husika.
   B Wahusika wa kazi husika.
   C Jina la kazi husika.
   D Jina la mtunzi wa kazi husika.
   E Mtindo wa kazi husika

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu ujenzi wa kazi ya kifasihi na lilimtaka mtahiniwa kubainisha jambo linalodhihirisha upekee wa kazi fulani za kifasihi. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *E Mtindo wa kazi husika* kwa kuwa walikuwa na uelewa kuwa mtindo ni *utendaji wa kipekee wa mtu, kikundi au jamii ya watu unaowezesha kujitofautisha na wengine*. Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri vipengele vyote na kupata alama zote za swali hili.

| | SEHEMU A | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
| | D | A | C | B | A | C | D | B | E | E |

Kielelezo 1.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri Swali la 1*

Baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa umahiri kuhusu ujenzi wa kazi za kifasihi hivyo kuchagua vipotoshi A, B, C na D ambavyo havidhihirishi upekee wa kazi ya kifasihi. Kwa mfano, *muundo* huonesha msuko wa matukio unaoweza kufanana kati ya msanii mmoja na mwingine, *wahusika* ni viumbe au vitu vinavyojengewa visa katika kazi ya fasihi na *jina la kazi husika* au *jina la mtunzi wa kazi husika* hayaoneshi upekee katika kazi fulani ya kifasihi kwani huweza kufanana na majina ya kazi za mtunzi au wasanii wengine. Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili na kupata alama hafifu.


| 01 | i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | B | D | A | C | E | D | E | C | C | B |

Kielelezo 1.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu Swali la 1*

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uandishi* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kujieleza kwa ufasaha, mpangilio mzuri wa mawazo na kutumia misamiati kwa usahihi. Swali lilikuwa na jumla ya vipengele vitano vilivyomtaka mtahiniwa kuoanisha maana za dhana za uandishi zilizokuwa katika orodha A na dhana husika zilizokuwa katika orodha B na lilikuwa na jumla ya alama 5.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 423,895 sawa na asilimia 99.8 ya wote waliofanya mtihani. Swali hili lilijibiwa vizuri sana ambapo asilimia 80.2 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 2. Watahiniwa 247,586 (58.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 1.5 hadi 3; watahiniwa 92,409 (21.8%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5 na watahiniwa 83,931 (19.8%) walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.

Uchambuzi unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa (58.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa walikuwa na uelewa wa baadhi ya maana za dhana za uandishi zilizokuwa katika orodha A na kuweza kuoanisha na dhana husika ya uandishi katika orodha B. Aidha, watahiniwa wachache (21.8%) walijibu vizuri swali hili kwa kuoanisha kwa usahihi maana za dhana za uandishi na dhana husika walizopewa. Watahiniwa hao walionesha umahiri wa hali ya juu wa dhana mbalimbali za uandishi kama vile *mantiki*, *mkato*, *uandishi*, *wazo* na *aya* na kuweza kuoanisha na maana za dhana hizo kwa usahihi. Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote na kupata alama za juu.

| 2. | ORODHA A | i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ORODHA B | C | E | A | F | B |

Kielelezo 2.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika Swali la 2*

Hata hivyo, watahiniwa wachache (19.8%) walishindwa kuoanisha maana ya dhana za uandishi zilizokuwa katika orodha A na dhana husika katika orodha B. Watahiniwa hao walitoa majibu yasiyo sahihi katika vipengele vingi na kupata alama hafifu kutokana na kukosa uelewa wa dhana mbalimbali zilizotahiniwa katika swali hili. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi *D Insha* na *G kistari* ambavyo havikuhusiana na maana zote zilizotolewa katika orodha A. Hii ilitokana na kuchanganya dhana ya *mkato* na *kistari* ambapo 'kistari' hufafanua sentensi iliyotangulia na 'mkato' hufanya kazi ya kutenga maneno yaliyo katika orodha fulani. Kielelezo 2.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingi na kupata alama hafifu.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | i | ii | iii | iv | v |
| | B | F | D | E | A |

Kielelezo 2.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu Swali la 2*

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI


Sehemu B ilikuwa na maswali sita (6) yenye kuhitaji majibu mafupi na ilikuwa na jumla ya alama 40. Sehemu hii ilihusu mada za *Fasihi Simulizi, Uundaji wa Maneno na Mjengo wa Tungo, Maendeleo ya Kiswahili, Uhakiki wa Riwaya* na *Ufahamu.*

### 2.2.1 Swali la 3: Kuongeza Msamiati wa Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Kuongeza Msamiati wa Kiswahili* na mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno*. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kukumbuka njia za kuunda maneno mbalimbali ya Kiswahili. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja njia za uundaji wa maneno katika vipengele (a), (b), (c) na (d) na lilikuwa na jumla ya alama 4.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 397,520 sawa na asilimia 93.6 ya wote waliofanya mtihani. Swali lilijibiwa kwa kiwango cha

wastani ambapo asilimia 49.9 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Hili ndilo swali lililojibiwa kwa kiwango cha chini ikilinganishwa na maswali mengine yaliyojibiwa na watahiniwa katika mtihani huo. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 3:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 3. Watahiniwa 199,158 (50.1%) walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1; watahiniwa 101,367 (25.5%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4 na watahiniwa 96,995 (24.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 1.5 hadi 2.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa (50.1%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1 kwa kuwa walishindwa kutaja njia za uundaji wa maneno katika vipengele vingi. Hali hii ilitokana na watahiniwa hao kukosa maarifa kuhusu uundaji wa maneno ya Kiswahili ambapo baadhi yao walielezea maana ya maneno waliyopewa badala ya kutaja njia za uundaji wa maneno hayo. Njia hizo ni kama vile (a) *Amirijeshi*- njia ya miambatano, (b) *Kiswahili*- njia ya utohoaji, (c) *kifaru* – kufananisha umbo na (d) *chajio* – njia ya kufupisha kwa kudondosha baadhi ya herufi. Aidha, watahiniwa


wengine walibainisha matumizi ya maneno waliyopewa na kuelezea maneno hayo kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 3.1 ni mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kutaja njia za uundaji wa maneno yote aliyopewa katika swali hili.




Kielelezo 3.1: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya Swali la 3*

Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja njia za uundaji wa maneno kwa kuandika katika kipengele (a) cheo cha madaraka au uongozi wa *Amirijeshi*, (b) uwepo wa lugha ya *Kiswahili* kutokana na makutano ya watu, (c) mnyama aitwaye *Kifaru* na (d) hakutoa maelezo yoyote kuhusu neno *Chajio*, hivyo kupata 0.


Watahiniwa wachache (25.5%) waliweza kutaja njia sahihi za uundaji wa maneno katika vipengele vyote ambapo waliandika katika (a) *Amirijeshi* (miambatano), (b) *Kiswahili* (utohoaji), (c) *kifaru* (kufananisha umbo) na (d) *chajio* – (ufupishaji). Watahiniwa hao walionesha umahiri katika uundaji wa maneno ya Kiswahili na kupata alama za juu. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja kwa usahihi njia za uundaji wa maneno katika vipengele vyote.


03 Njia za kuanda maneno
a) Amirijeshi : Uambatanishaji
b) Kiswahili ; kutohoa maneno
c) kifaru : Mfananisho wa umbo
d) Chajio : Ufupishaji wa maneno.

Kielelezo 3.2: *Sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa katika Swali la 3*

Kielelezo 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja kwa usahihi njia za uundaji wa maneno *amirijeshi*, *Kiswahili*, *kifaru* na *chajio* kulingana na matakwa ya swali na kupata alama za juu.

Hata hivyo, watahiniwa wengine (24.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa walitaja kwa usahihi njia za uundaji wa maneno kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Kielelezo 3.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine.



3 a/ Amirijeshi
Njia ya miambatano au kuangunisha maneno
Amiri + Jeshi

b/ Kiswahili
Njia ya kufananisha jina la mtu, ambaye ni mswahili anayeishi pwani ya afrika mashariki na anazungumza lugha ya Kiswahili

c/ Kifaru
Njia ya kufananisha sura na umbo la kitu, hii kimeitwa kifaru kwa kufanana na mnyama kifaru


d/ Chajio
Njia ya kufananisha matumizi ya kitu.

Kielelezo 3.3: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetoa majibu yasiyojitosheleza katika Swali la 3*

### 2.2.2 Swali la 4: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi*. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua tungo za kifasihi na zisizo za kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika nahau zenye maana sawa na tungo alizopewa katika kipengele (a) hadi (d) na lilikuwa na jumla ya alama 4.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 404,125 sawa na asilimia 95.1 ya wote waliofanya mtihani. Swali lilijibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo asilimia 64.0 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 4:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 4. Watahiniwa 169,733 (42.0%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4; watahiniwa 145,889 (36.0%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1 na watahiniwa 88,908 (22.0%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 1.5 hadi 2.5.

Watahiniwa 169,733 sawa na asilimia (42.0%) walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kutokana na kuandika kwa usahihi nahau zenye maana sawa na tungo walizopewa katika vipengele (a) hadi (d). Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutambua nahau zinazotumika katika lugha ya Kiswahili, hivyo waliweza kulinganisha nahau husika na tungo walizopewa. Watahiniwa hao waliweza kuandika nahau zenye maana sawa na tungo (a) Jumanne ni kijana mchoyo kuwa *Jumanne ana mkono wa birika*, (b) Yule ni mropokaji sana kuwa *Yule ni domo kaya*, (c) Malingumu ni mwizi kuwa *Malingumu ana mkono mrefu* na (d) Mwalimu wetu ameoa kuwa *Mwalimu wetu amepata jiko*. Kielelezo 4.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi swali hili.

| | |
|---|---|
| 4 | (a) Sumanne anamkono wa birika. |
| | (b) Yule ni domo kaya. |
| | (c) Matingumu anamkono mrefu. |
| | (d) Mwalimu amepata jiko. |
| | |

Kielelezo 4.1**:** *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri Swali la 4*

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika kwa usahihi nahau zenye maana sawa na tungo alizopewa katika vipengele (a) hadi (d) na kupata alama za juu.


Aidha, asilimia 36.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 1 kwa kuwa hawakuweza kuandika nahau zenye maana sawa na tungo walizopewa, badala yake waliandika *methali, misemo, vitendawili* na *tanzu* nyingine zisizohusiana na nahau na kupata 0. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja methali badala ya nahau na kupata 0.

| | |
|---|---|
| 4. | a) Mchagua nazi huangukia koroma. |
| | |
| | b) Haba na haba hujaza kibaba. |
| | |
| | c) Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. |
| | |
| | d) Pole pole ndio mwendo. |
| | |

Kielelezo 4.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya Swali la 4*

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika nahau katika vipengele (a) hadi (d) kwa kuandika methali kinyume na matakwa ya swali, hivyo kupata alama hafifu.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa (22.0%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa kuandika baadhi ya nahau zenye maana sawa na tungo walizopewa kwa usahihi na kushindwa katika tungo nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuandika nahau zenye maana sawa na tungo (a) na (c) na kushindwa katika vipengele (b) na (d). Kielelezo 4.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vingine.


4. Jumanne ni kijana mchoyo.
(a) Anamkono wa birika
(b) Yule ni mropokaji sana.
Anamdomo wa chiriku.
(c) Malingumu ni mwizi.
Anamkono mrefu.
(d) Mwalimu wetu ameoa.
Amevunja jiko

Kielelezo 4.3: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani katika Swali la 4*


Kielelezo 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika nahau sahihi kwa tungo (a)….*ana mkono wa birika* na (c) ....*ana mkono mrefu* ambapo katika tungo (b) na (d) aliandika misemo kinyume na matakwa ya swali na kupata alama za wastani.

### 2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno na Mjengo wa Tungo

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi* na mada ndogo za *Uundaji wa Maneno* na *Mjengo wa Tungo*. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuunda nomino mbili kwa kila kitenzi alichopewa kwa kutumia mnyumbuliko katika kipengele (a) na (b) kutunga tungo kwa kuzingatia viambajengo alivyopewa kwa kila kipengele. Swali hili

lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuunda maneno/tungo na lilikuwa na jumla ya alama 8.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 418,642 sawa na asilimia 98.5 ya wote waliofanya mtihani. Swali lilijibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo asilimia 53.6 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 5:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 5. Watahiniwa 194,250 (46.4%) walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2; watahiniwa 141,920 (33.9%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 82,472 (19.7%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo chini ya nusu ya watahiniwa (46.4%) walipata alama hafifu 0 hadi 2. Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa kuhusu uundaji wa maneno na kutumia viambajengo katika utunzi wa tungo. Watahiniwa hao katika kipengele (a), waliweka viambishi awali katika vitenzi ambapo waliandika katika (i) piga – *anapiga, atapiga.*…badala ya kunyumbua vitenzi hivyo

ili kupata nomino. Hali kadhalika, wengine walinyumbua vitenzi hivyo ili kupata kauli mbalimbali kama vile (iv) cheza – *anachezea, anachezewa,…* kinyume na matakwa ya swali. Aidha, katika kipengele (b) watahiniwa hao walishindwa kutunga tungo kwa kuzingatia viambajengo walivyopewa kwa kila kipengele, hivyo kupata alama za chini. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kinyume na matakwa ya swali.



5 i) Piga – pigwa, pigana
ii) Lima – Limiwa, Limianeni
iii) pika – pikiwa, pikianeni
iv) Cheza – Chezeni, Chezewa


(b)
(i) Simu yetu imeibiwa
(ii) nanuka mtaro
(iii) Simu yangu
(iv) Nimekamatwa kimeibwa nakwenda polisi kufungwa

Kielelezo 5.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya Swali la 5*

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuunda nomino mbili kwa kila kitenzi (i) hadi (iv) katika kipengele (a) na kutunga tungo zisizo sahihi kulingana na viambajengo (i) hadi (iv) alivyopewa katika kipengele (b).

Licha ya kiwango hicho kuwa cha chini katika swali hili, asilimia 33.9 ya watahiniwa hao walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya

vipengele vya swali hili. Baadhi yao waliweza kujibu kipengele kimoja kati ya (a) au (b) kwa usahihi na kushindwa katika kipengele kingine. Kielelezo 5.2 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili katika kipengele (a) na kupata alama za wastani.




5a)
i) • Pigika
• Pigia
ii) • Limwa
• Limika.
iii) • Pikika
• Pikana
iv) • chezeka
• Chezwa

Kielelezo 5.2: *Sampuli ya jibu baya la mtahiniwa katika Swali la 5(a)*

Kielelezo 5.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuunda nomino mbili kwa kila kitenzi alichopewa katika kipengele (a) kwa kuandika kauli mbalimbali za vitenzi hivyo na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (19.7%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kuwa waliweza kuunda nomino mbili kwa kila kitenzi katika kipengele (a) (i) hadi (iv) na kutunga tungo kwa kuzingatia viambajengo (i) *kishazi tegemezi* + *kishazi huru*, (ii) *kishazi huru*, (iii) *kishazi tegemezi* na (iv) *kishazi huru* + *Kishazi huru* kwa usahihi katika kipengele (b). Kielelezo 5.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kuzingatia matakwa ya swali.




Kielelezo 5.3: *Sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa katika Swali la 5*


Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeunda nomino mbili kwa kila kitenzi alichopewa na kutunga tungo sahihi kulingana na viambajengo alivyopewa kwa kila kipengele.

### 2.2.4 Swali la 6: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* na mada ndogo za *Asili ya Kiswahili* na *Kukua/Kuenea kwa Kiswahili*. Swali hili lilimtaka mtahiniwa katika kipengele (a) kufafanua vipengele vinne vinavyodhihirisha uhusiano baina ya Kiswahili na lugha za Kibantu na katika (b) kueleza mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi za Waarabu katika dini na biashara. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kukumbuka historia

mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lilikuwa na jumla ya alama 8.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 408,294 sawa na asilimia 96.1 ya wote waliofanya mtihani. Swali lilijibiwa kwa kiwango cha wastani ambapo asilimia 56.6 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 6:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 6. Watahiniwa 177,200 (43.4%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2; watahiniwa 167,401 (41.0%) kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 63,694 (15.6%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo watahiniwa 177,200 sawa na asilimia 43.4 walijibu swali na kupata alama hafifu 0 hadi 2. Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa katika kufafanua uhusiano uliopo kati ya lugha ya Kiswahili na Kibantu. Pia, watahiniwa hao walishindwa kueleza mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi za Waarabu katika dini na biashara. Kutokana na kukosa weledi huo,

baadhi ya watahiniwa waliezea *chimbuko la lugha ya Kiswahili* na wengine walibainisha *lahaja mbalimbali* zilizokuwa zinaongelewa katika maeneo mbalimbali. Aidha, baadhi yao walitoa sababu za *uteuzi wa kiunguja* katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili kinyume na matakwa ya swali. Watahiniwa hao walitakiwa kuthibitisha uhusiano kati ya lugha ya Kiswahili na Kibantu kama vile *muundo wa sentensi unaofanana, msamiati, upatanisho wa kisarufi* na *vitenzi vya lugha ya Kiswahili vinavyoanza na viambishi vya nafsi*. Pia, walishindwa kuainisha mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi ya waarabu kwa kukosa maarifa kuhusu kukua na kuenea kwa Kiswahili katika biashara na dini. Kiuhalisia d*ini ya Kiislam* ilitumia lugha ya Kiswahili katika mahubiri yake. Katika *biashara* baadhi ya misamiati ilizuka na hatimaye iliingizwa kwenye lugha ya Kiswahili, kama vile *thamani, hasara, kodi, thumni na thelathini*. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.


6 a) i) amelala.
ii) agonili.
iii) yogonile.
iv) yaganila.
b) i) Dini
Waarabu walipofika nchi walitumia kiswahili
katika kueneza dini ya kiislamu hasahasa
miji iliyokuwa ngambo ya bahari na visiwani.
kiswahili kilitumika katika kuelekeza watu yingi
dini iliyoko na umuhimu katika maisha yetu.
6) ii) Biashara
Pia, waarabu walifanya chughuli za kibiashara kwani ndicho kitu muhimu walichokuja
kukufanya hivyo basi walibidi wajifunze kiswahili
ili iliwaweze kufanya chughuli za kibiashara.
Na hivyo waliweza kueneza kiswahili na hata
kukisambara.

Kielelezo 6.1: *Sampuli ya majibu mtahiniwa yasiyo sahihi katika Swali la 6*

Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua uhusiano uliopo kati ya lugha ya Kiswahili na Kibantu. Mtahiniwa huyo alinakili tungo alizopewa katika kipengele (a) na kutoa maelezo yasiyojitosheleza katika kueleza mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi za Waarabu katika dini na biashara katika kipengele (b), hivyo kupata alama hafifu.

Aidha, asilimia 41.1 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi za Waarabu kama vile *kutumika katika dini ya kiislamu*, *kuongezeka kwa msamiati wa Kiswahili* kutokana na kutumika katika biashara na kuzalisha maneno kama vile thamani, thelathini, thumni, faida, kodi na hasara. Hata hivyo, watahiniwa hao walishindwa kufafanua baadhi ya vipengele vinavyodhihirisha uhusiano baina ya lugha ya Kiswahili na lugha za kibantu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) alifafanua vizuri vipengele vitatu vya uhusiano baina ya Kiswahili na lugha za kibantu na katika kipengele (b) alielezea mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi za waarabu bila maelezo ya kutosha na mifano, hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (15.6%) walifaulu kwa kiwango cha juu kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili na mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika utawala wa Waarabu. Watahiniwa hao waliweza kufafanua vipengele vinne vilivyodhihirisha uhusiano baina ya Kiswahili na lugha za kibantu kwa kuandika katika kipengele (a) (i) *mpangilio wa tungo za Kiswahili na kibantu hufanana yaani zote zina muundo wa nomino na kitenzi (N + T),* (ii) *Msamiati unaofanana* (iii) *Upatanisho wa kisarufi unaofanana* yaani viambishi vyenye upatanisho wa kisarufi katika sentensi ni *nomino* na *kitenzi* chake. Katika kipengele cha (iv) Vitenzi vya lugha ya Kiswahili huanza na viambishi vya nafsi mfano, **a**melala – Kiswahili, **a**gonile – Kingoni. Katika kipengele (b) walieleza kwa usahihi mafanikio ya lugha ya Kiswahili enzi za Waarabu, kama vile *kutumika katika dini ya Kiislam*; *kukua kwa msamiati wa lugha ya Kiswahili* na *kutumika katika shughuli za biashara*. Kielelezo 6.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

06 (a) I. Msamiati
– Msamiati wa lugha ya Kiswahili na lugha ya kibantu vinaendana au vinafanana baina yao. Kwa mfano.

| lugha | neno |
|---|---|
| Kiswahili | mtoto |
| Kingoni | mwana |
| Kigogo | mwana |
| Kihaya | omwana. |

II. Mnyumbuliko wa vitenzi.
– katika mnyumbuliko wa vitenzi lugha ya Kiswahili na ile ya kibantu hufanana kwa

06 (a) kuangalia viambishi au kauli
Mfano.

| lugha | Neno |
|---|---|
| Kiswahili | lala |
| Kingoni | goni |
| Kigogo | gorile |
| Kihaya | nagila |


III. Upatanisho wa kisarufi.
– Sarufi ya lugha ya Kiswahili na ile ya lugha ya kibantu huelekeana kufanana
Mfano;

| lugha | sentensi |
|---|---|
| Kiswahili | mtoto amelala |
| Kingoni | Mwana agonile |
| Kigogo | Mwana yagonile |
| Kihaya | Omwana yanagila. |

IV. Mnyumbuliko wa vitenzi.
– Lugha ya kibantu na lugha ya Kiswahili mnyumbuliko wake wa vitenzi huendana
Mfano;

| Lugha | tend | tendesha | tendeka |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | cheka | chekesha | chekeka |
| Kinyakyusa | neka | nekesya | iseko |
| kijita | seka | sekesya | sekeka |
| Kihaya | kweka | sekesha | kwekeka |

(b) I. Dini
Waarabu walipokuja katika pwani ya Afrika ya Mashariki walikuja pamoja na kueneza lugha na dini ya Kiislamu.



06(b) katika kuenezo uislamu walifanya vitu vingi
Mfano; i. Walifundisha watu namna ya kusoma na kuandika lugha ya kiarabu ambayo ilichangia kwa ungezeko la msamiati ya lugha ya kiswahili. Mfano neno kama vile. utajiri

2. Lakini pia waliweza kuleta msamiati mipya ya lugha ya Kiswahili.


ii. Biashara
- Katika biashara Waarabu walifanya mambo mengi sana hapo nchini.
Mfano:
- Biashara ya karafuu iliyoanzishwa na Waarabu waliweza kuimarisha maganiko ya lugha ya Kiswahili.

Kielelezo 6.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri Swali la 6*

### 2.2.5 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Riwaya* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi mambo manne ya kufanana kati ya mhusika *Sekai* na *Mama N'tilie* kuhusu wasifu wao wa ndani na lilikuwa na jumla ya alama 8.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 394,108 sawa na asilimia 92.8 ya wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana ambapo asilimia 84.4 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha viwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ambapo, watahiniwa 214,001 (54.3%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8; watahiniwa 119,021 (30.1%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 61,481 (15.6%) walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.

Zaidi ya nusu ya watahiniwa (54.3%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu ambazo ni 5.5 hadi 8. Watahiniwa hao walitoa majibu yaliyojitosheleza kuhusu kufanana kwa wahusika Sekai na Mama N'tilie kwa kuzingatia wasifu wao wa ndani. Watahiniwa hao waliweza kufafanua mambo manne ya kufanana ambayo yalijitokeza kwa wahusika hao. Mambo hayo ni *uvumilivu*, *huruma*, *mapenzi ya dhati na uchapakazi*. Aidha, walibainisha kwa usahihi wahusika hao ambao kwa jinsi ni wanawake, *Sekai* kutoka katika riwaya ya "Takadini" na *Mama N'tilie* kutoka katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie." Wahusika wote walionesha upambanaji wa hali ya juu pamoja na kwamba kila mmoja alikumbana na mazingira magumu kwa wakati tofauti ambapo maudhui ya watunzi yanaonekana kupitia wahusika hao wakuu. Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

7. Kutoka katika riwaya ya "Takadini" na "Watoto wa Mama Ntilie". Zifuatazo ni sifa za ndani ambazo huwafananisha "Sekai" na "Mama Ntilie"

i) Uvumilivu

Hii ni sifa ambayo Sekai alikuwanayo hasa kwa kipindi chote alichokuwa hajapata mtoto Sekai aliweza kuvumilia kejeli za wake wenza Badirai na Rumbidzai. Lakini pia Mama Ntilie alikuwa muvumilivu kwa mumewe Mzee lomolomo japo mzee huyu alikuwa mlevi kupindukia lakini Mama Ntilie alimvumilia kwa bila jambo.

ii) Mapenzi ya dhati

Hii pia ni sifa ambayo huwafananisha Sekai na Mama Ntilie. Sekai alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Mumewe Mzee Makwati japokuwa Makwati alioa wake wengi lakini Sekai alimpenda. Pia Sekai alikuwa na Mapenzi ya dhati ya mtoto wake Takadini. Lakini pia Mama Ntilie alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Mumewe lomolomo pamoja na watoto wake Mama Ntilie alimpenda Mzee lomolomo kwa dhati japokuwa Mzee lomolomo alikuwa Maskini na Mlevi lakini alimpenda hivyohivyo.

iii) Huruma

Sekai alikuwa na huruma kwa Mtoto wake ndio maana aliamua kutoroka kijijini ili kunusuru maisha ya Takadini. lakini Pia Mama Ntilie alionyesha kuwa na Huruma na kuamua kumchukua kurwa ambaye ni mtoto yatima na wa mtaani na kuamua kuishi nae kama mtoto wake.

iv) Uchapakazi

Sekai alikuwa mchapakazi na kuleta maendeleo katika kijiji alichokimbilia ili kumuokoa mtoto wake Sope (Takadini). Pia Mama Ntilie alikuwa akijianya kazi kwa bidii ili jamilia yake iwe vizuri jambo ambalo alikuwa akilifanyia kwa bidii.

Kielelezo 7.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi Swali la 7*

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi wasifu wa ndani wa kufanana kati ya wahusika Sekai na Mama N'tiliye. Wasifu huo ni kama vile *uvumilivu*, *mapenzi ya dhati*, *huruma* na *uchapakazi*, hivyo kupata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 119,021 sawa na asilimia 30.1 kati ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama za wastani 2.5 hadi 5 kwa kuwa hawakuweza kuelezea mambo manne ya kufanana kuhusu wasifu wa ndani wa wahusika *Sekai* na *Mama N'tilie*. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kueleza baadhi ya wasifu wa ndani wa wahusika na kufanana kwao. Wengine walieleza baadhi ya wasifu na kushindwa kueleza sifa nyingine zilizokuwa zinawafananisha wahusika hao. Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kujibu vizuri baadhi ya hoja na kushindwa kueleza vyema hoja nyingine.

7. Katika Riwaya ya Takadini na Watoto wa Mama Ntilie wameweza kuchorwa katika picha au mwonekano mbalimbali unaofanana kama ifuatavyo

(i) Wanawake kwa wote wawili wameweza kuchorwa kama wakombozi wa kiuchumi. Hapa tunawaona wanawake kwa ambaye ni Sekai na Mama Ntilie wakijihusisha na shughuli mbalimbali katika jamii. Mfano Sekai anaonekana ni mkulima na mtu anayejituma kwenye mambo ya shambani. Pia tunamwona Mama Ntilie akijihusisha na shughuli za uuzaji wa chakula na genge kwa ajili ya kupata kipato yeye na familia yake.

(ii) Wanawake kwa wamechorwa walezi / wazazi wa kulinda familia zao majumbani. Hapa tunamwona Mama Ntilie akihudumia familia yake peke yake ikiwa mumewe anajihusisha na ulevi. Pia kwa Sekai amekuwa kama mtu asiye na mume pale anapomlea Takadini peke yake.

(iii) Wanawake kwa wamechorwa kama watu dhaifu wasio na sauti mbele za wanaume zao. Hii tunaiona kwa Sekai pale anapojifungua Takadini na analazimishwa kwamba Takadini anatakiwa auawe bila yeye kupinga kitu chochote. Pia kwa Mama Ntilie pale anaposhindwa kumzuia mumewe kuhusu suala la ulevi.


(iv) Sekai na Mama Ntilie wote wameonekana kama watu majasiri kwa sababu ya kupambana na vikwazo na matatizo yote yanayowakumba. Mfano Sekai pale anapotoroka kijijini kwao na kwenda kuishi msituni na kuhama kijiji kabisa kwa sababu ya kumlinda mwanawe aitwaye Takadini.

Kielelezo 7.2 : *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye majibu yasiyojitosheleza katika swali la 7*

Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza wasifu wa wahusika usio sahihi, kama vile *udhaifu* badala ya ujasiri. Pia

mtahiniwa huyo hakutoa maelezo ya kutosha kuhusu ujasiri wa mhusika Mama N'tilie, hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (15.6%) walipata alama hafifu 0 hadi 2 kwani hawakuweza kueleza wasifu wa ndani wa wahusika *Sekai* na *Mama N'tilie* kwa namna wanavyofanana. Baadhi ya watahiniwa walielezea mambo yasiyo sahihi kuhusu wasifu wa ndani wa wahusika hao. Mambo hayo ni kama vile *uvivu, wizi, umalaya* na *mengine* yasiyohusiana na sifa za wahusika hao. Wengine, kutokana na kutokuwa na uelewa wa riwaya hizo, walielezea mambo yanayopatikana katika vitabu vya tamthiliya na ushairi, kama vile *maambukizi ya VVU UKIMWI* (Kilio Chetu) na *matabaka* (Wasakatonge). Kielelezo 7.3 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.


7. i) Jambo la kwanza Sekai na mama ntilie wote walikuwa maskini ndio jambo lililowafanya wengine watoto wao wanafishwe shuleni na chikoya na wengine kukatatiwa na mume zao mfano Sekai kwa ajili ya kumzaa (Zeru Zeru).

ii) Jambo lingine la Sekai na mama ntilie kufanana ni kwa upande wa imani potofu kwa sababu wote walikuwa wanaamini imani za kishirikina.

iii) Jambo lingine la wahusika wote kufanana ni walikuwa jinsia moja yaani wanawake kwa Sekai katika riwaya ya Takadini aliyepata mtoto (Zeru Zeru) pia mama ntilie ambaye watoto wake wamenyishwa shule kisa nguo zao kuchanika au sare kiujumla.

iv) Jambo lingine la wahusika hawa kufanana ni wote wameonyeshwa kama chombo cha starehe na chombo duni katika riwaya zote sababu za wahusika kufananishwa.


Kielelezo 7.3: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyokidhi katika Swali la 7*

Kielelezo 7.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza wasifu wa ndani wa wahusika *Sekai* na *Mama N'tilie*. Badala yake alieleza dhamira zisizowafananisha wahusika hao, kama vile *chombo cha starehe* na *wenye imani za kishirikina*, hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.6 Swali la 8: Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kujenga ufahamu wa kifungu cha habari. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari, kisha kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Swali lilikuwa na vipengele (a) – (d) lenye jumla ya alama 8.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 408,895 sawa na asilimia 96.2 ya wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 81.2 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 8:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 8. Watahiniwa 177,446 (43.4%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 5.5 hadi 8; watahiniwa 154,562

(37.8%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2.5 hadi 5 na watahiniwa 76,872 (18.8%) walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.

Watahiniwa 177,461 (43.4%) waliojibu vizuri swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama za juu 5.5 hadi 8 kwa kuwa walijibu vizuri vipengele vingi vya swali. Watahiniwa hao waliweza kuhusisha kifungu cha habari walichokisoma katika kujibu maswali waliyopewa katika kipengele (a) – (d) kwa usahihi. Katika kipengele (a), waliweza kupendekeza kichwa cha habari, kama vile USHUJAA WA SONI/MSIMAMO WA SONI/MILA POTOFU. Katika kipengele (b) walitoa sababu za Soni kutoroka nyumbani kwake na kukimbilia msituni kuwa ni *kuepusha kifo cha mwanae* ambaye rangi yake ilikuwa tofauti na watoto wengine. Katika kipengele (c), walieleza ni kwa jinsi gani mwandishi wa habari anavyoichukulia jamii ya akina Soni kuwa ni yenye imani potofu. Kwa mfano, wanapotaka kumuua mtoto wa Soni kwasababu ya utofauti wa rangi ni ukiukwaji wa misingi ya haki za binadamu. Isitoshe, katika kipengele (d), walieleza kwa usahihi nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kutoa hoja mbili, kama vile *mtu mwenye msimamo* kwani mhusika Soni ni mwanamke aliyemtetea mwanae asiuawe licha ya kuwa na kasoro na kukataliwa na jamii yake; *mtu jasiri* kwa kuwa alithubutu kutembea msituni peke yake akiwa na mkuki na ngao tayari kwa kupambana na adui awe mnyama au binadamu. Kielelezo 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi kipengele (a) – (d) na kupata alama za juu.


8. a) MILA POTOFU.

b) Soni alitoroka nyumbani kwake na kukimbilia mafichoni kwa sababu sehemu alipokuwa akiishi soni walitaka kumuua mwanake kwasababu alikuwa Ana rangi tofauti na wengine.

c) Mwandishi wa Habari hii anawachukulia jamii ya akina soni, Ni watu wanao amini Mila potofu.

d) kutokana na habari niliyosoma, Nafasi ya mwanamke katika jamii:

i) Mwanamke ni Mlezi wa Familia; Ni kweli kabisa tunaona Soni alikuwa ni Mama wa Tumaini.


ii) Mwanamke ni Jasiri: Ni kweli kabisa tunaona Soni alipigania Maisha ya Mwanake kwa kumuepusha na Mauaji. kutokana na Utofauti wa rangi alikuwa nao mtoto Tumaini.

Kielelezo 8.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri Swali la 8*

Kielelezo 8.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyesoma kifungu cha habari kwa ufahamu na kuweza kupendekeza kichwa cha habari; kutoa sababu za Soni kutoroka nyumbani kwake; kueleza mtazamo wa mwandishi kuhusu jamii ya akina Soni na; kueleza nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kutoa hoja mbili kwa usahihi.

Aidha, asilimia 37.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu swali hili aliweza kujibu baadhi ya vipengele na kukosa vingine kutokana na kukosa ufahamu wa kutosha wa kifungu cha habari. Hivyo alipendekeza kichwa cha habari kisichokidhi mawazo makuu yaliyo katika habari kwa kuandika “KUTOROKA KWA SONI” badala ya USHUJAA WA SONI/MSIMAMO WA SONI na kufafanua nafasi ya mwanamke

kama *chombo cha starehe* badala ya mtu mwenye msimamo na shujaa. Kielelezo 8.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu baadhi ya vipengele, hivyo kupata alama za wastani.


8. (a) KUTOROKA KWA SONI

(b) Soni alitoroka nyumbani kwake kwenda msituni kwa kuwa alikuwa analinda maisha ya mtoto wake aliyekuwa anaenda kuuliwa kutokana na utofauti wa mtoto wake kama mwandishi anavyosema,
"Mtoto alikuwa karibu sawa na wengine kuliko tofauti yake ni rangi tu. Sasa mbona wanataka kumuua".

(c) Jamii ya Soni inafuatilia mila na desturi mbovu na mbaya.


(d) Mlezi bora, Soni alimpenda mtoto wake - Tumaini nae akaamua kulinda maisha yake kwa kumtorosha ili asiuliwe. Alimbeba na kumnyonyesha mtoto wake kwa upendo mkubwa bila ya kujilaumisha. Amesimama kama mlezi pekee na mzazi pekee.

Chombo cha starehe, Soni amefumika kama chombo cha starehe kwa mume wake kwa kuwa amesimama kama katumiwa na mtoto aliyezaliwa hafahamu hii ndo nyendo nzuri katika maisha kwa kuwa inavunjisha moyo kwa wengine. Hivi ndivyo waraa wake wanachukuliwa katika jamii.

Kielelezo 8.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza katika Swali la 8*

Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 18.8 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2 kwa kuwa

walishindwa kutoa majibu katika vipengele vingi. Watahiniwa hao walishindwa kupendekeza kichwa cha habari; walishindwa kueleza sababu za Soni kutoroka nyumbani na kukimbilia msituni; walishindwa kueleza mtazamo wa mwandishi na kuonesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Watahiniwa hao walitakiwa kupendekeza kichwa cha habari katika (a) *USHUJAA WA SONI/MSIMAMO WA SONI*; (b) kutoa sababu za Soni kutoroka nyumbani kwake ambazo ni pamoja na *kumnusuru mwanae dhidi ya kifo*; (c) kueleza mtazamo wa mwandishi kuhusu jamii ya akina Soni kuwa ni *jamii yenye imani potofu zilizopitwa na wakati* na; kuelezea nafasi ya mwanamke katika jamii, kama vile *mtu mwenye msimamo, shujaa, mpambanaji na mwenye huruma*. Kielelezo 8.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyokidhi maswali yaliyotokana na kifungu cha habari.


08 (a) SAFARI YA SONI
(b) Kwa sababu, alikuwa anataka kumtafuta baba yake. wakati yeye alikuwa anapotea
(c) Mwandishi anachukulia jami ya akina Soni ni ya kimaskini
(d) i. Mwanamke anachorwa kama mtu mwoga
ii. mwanamke anachorwa kama mtu anayohitaji msaada kwa mambo mbalimbale

Kielelezo 8.3: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu Swali la 8*

Kielelezo 8.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 8 kwa kuandika katika (a) kichwa cha habari *SAFARI YA SONI*, (b) sababu za Soni kutoroka nyumbani kwake kuwa ni 'kutaka kumtafuta baba yake', (c) maelezo ya mtazamo wa mwandishi kuhusu jamii ya akina Soni kuwa ni 'jamii ya kimasikini' na (d) alielezea nafasi ya mwanamke katika jamii kuwa ni 'mtu mwoga' kinyume na ujumbe uliopo katika kifungu cha habari, hivyo kupata alama hafifu.


### 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu C ilikuwa na maswali manne ambayo yalimhitaji mtahiniwa kujibu maswali matatu (3) ambapo kila swali lilikuwa na alama 15 na kufanya jumla ya alama 45 katika sehemu hii.

#### 2.3.1 Swali la 9: Uandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha ya kisanaa yenye maneno 200 na yasiyozidi 250 yenye kutumia kauli mbiu "Watoto zingatieni daima maonyo ya wazazi wenu" na yenye kuishia na methali isemayo "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu." Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa la kuchagua ambapo zaidi ya nusu ya watahiniwa, yaani 226,145 sawa na asilimia 53.2 walilijibu. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo, asilimia 66.1 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





Chati Na. 9: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 9. Watahiniwa 124,832 (55.2%) walifaulu kwa kiwango

cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5; watahiniwa 76,663 (33.9%) walikuwa na kiwango hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4 na watahiniwa 24,650 (10.9%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15.

Zaidi ya nusu ya watahiniwa (55.2%) waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kuandika insha ya kisanaa yenye kichwa cha habari “MAONYO YA WAZAZI” au “WATOTO WASIKILIZENI WAZAZI WENU.” Aidha, baadhi ya watahiniwa waliandika insha ya hoja badala ya insha ya kisanaa kutokana na kushindwa kutumia lugha ya kisanaa ili kushadidia maelezo yao. Wengine, waliandika insha isiyozingatia mambo yote muhimu, yaani kuwa na utangulizi usiojitosheleza, kutopanga hoja kimantiki na kutotumia maneno ya kuvutia na yenye idadi isiyokidhi matakwa ya swali. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.




09 WATOTO ZINGATIENI MAONYO YA WAZAZI

Maonyo, ni mambo ambayo mtu hupewa ili kuepeshwa na hatari fulani katika maisha. wazazi wengi wamekuwa wakitoa maonyo kwa watoto wao ili kuwaepusha watoto na shida mbali mbali.

Maonyo ambayo wazazi hutoa kwa watoto wao huwa afali ya kuwaepusha na matendi mabaya. wazazi wengi huwaasa watoto kuepukana na matendi yasiyo lota tija maishani mwao ili kuishi maisha mazuri.

Vito vito wazazi hutoa maonyo kwa watoto ya kutokujihusisha na mapenzi katika


09 umri mdogo walokuwa nao ili kupata kuwaepusha
watoto hawa na mimba za utotoni wakiwa
masomoni
Wazazi huwaonya sana watoto wao katika
masuala ya kuepukana na masaibu ya utanda
wazi. utandawazi ni suala ambalo linathiri sana
akili za watoto wengi hivyo wazazi hutoa
mafundisho ili kuwajenga watoto kiakili na
maadili mema.
Vile vile wazazi watoa maonyo mengi
kwa watoto kuhusu kupuuza elimu. Elimu
ni jambo muhimu sana kwa mtoto ambalo
anabidi alipate. ambalo wazazi wengi sana
wamo tilia mkazo jambo hili lakini watoto
wengi wanaonekana kulipuuzia sana.
Wazazi huwaonya sana watoto wao
katika suala la mavazi. wazazi wengi
wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana kwa
kuwapa watoto maonyo juu ya mavazi
wanayoyavaa kwani yanawapa kuwaletea shida
hivyo basi watoto wanapaswa kuyazingatia
yote ambayo wanaambia na wazazi wao.
Hivyo basi, Maonyo haya yote wanayo
walio kuwa wanayotoa kwa watoto ni
kwa ajili tu ya kusaidia na kuhakikisha
maisha bora ya watoto wao, malezi na
makuzi bora wanavyo kuwa, Hivyo basi
asiepokea na kuzingatia malezi haya huishia
pabaya siku zote kwani "asiyesikia la
mkuu huvunjika guu".

Kielelezo 9.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha isiyojitosheleza katika swali la 9*

Kielelezo 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha isiyojitosheleza kwa kuandika insha ya hoja badala ya insha ya kisanaa. Hata hivyo, mtahiniwa huyo aliweza kupanga mawazo katika mtiririko na kutoa hitimisho lenye methali "Asiyesikia la Mkuu huvunjika guu" na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache (10.9%), walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kuanzia 10 hadi 15 kwa kuwa waliweza

kuandika insha ya kisanaa kwa kuzingatia *kichwa cha habari* “MAONYO YA WAZAZI” au “WATOTO WASIKILIZENI WAZAZI WENU”, *muundo rasmi wa insha*, *lugha ya kisanaa*, *mtiririko wa mawazo* na *idadi ya maneno*. Katika kiini, waliweza kubainisha tabia isiyokubalika katika jamii, kama vile kushiriki ngono zembe na kupata mimba zisizotarajiwa na kuleta madhara kama vile kukatisha masomo. Aidha, waliweza kutumia taratibu anuai za uandishi na katika hitimisho walimalizia kwa methali, “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu”, hivyo kupata alama za juu. Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha kwa usahihi kulingana na matakwa ya swali.

9. WATOTO ZINGATIENI MAONYO YA WAZAZI


Familia ya Mzee Athanas Kamata na Mkewe Joyce Samwel walijulikana katika kijiji cha Songambele na Mungu aliwajaalia mtoto mmoja wa kike aitwae Anna na wa kiume aitwae Matanga. Watoto walikuwa ni watiifu sana kwani walitoa salamu kwa watu bila kukosesha mtu.

Siku zilienda, miaka ikapita, mara mtoto wao wa kike akapata nafasi ya kwenda kusoma India kozi ya Udaktari ambapo wote familia nzima walifurahi sana na hivyo walimfanyia sherehe Anna. Siku zilikaribia za kuelekea nchini India, mdada huyu alijiandaa vema sana kwa ajili ya kwenda kupata kozi ile.

Siku iliwadia ya Anna kuondoka lakini kabla hajaondoka baba yake alimwita pamoja na mama yake ili wapate kumpatia mausia ya mwisho ambayo yangepata kumsaidia katika maisha yake kipindi anasoma India na baba alimwambia yafuatayo;

Mtangulize Mungu, alimsihi binti yake apate kuwa binti mwema ambaye anampenda Mungu pamoja na kuzishika amri zake, lakini pia alimwambia penda kusaidia wahitaji kwani hujui ya leo na ya kesho yatakuwaje kwa hivyo ukimwona mtu anayehitaji usisite kupata kumsaidia.

Lakini kikubwa na cha mwisho, alichomsihi binti yake kabla hajaondoka alimwambia na kumsihi kwamba asome kwa bidii lakini asijihusishe na mapenzi kwani alikuwa bado ni mtoto mdogo sana!


9. Muda na wazazi ambao Anna alimsubiri ulikuwa ni kupanda ndege na kuondoka kwani alionekana kuchoka kusikiliza mashauri kutoka kwa wazazi wake. Ndege ilitua na ndipo mama na baba yake walimuaga, kwa mara ya mwisho na akaanza safari ya kuelekea India.

Punde si punde binti alifika jijini India na hapo ndipo maisha yake ya chuoni yalipoanza, na kwa kweli Anna alikuwa mzuri na hakukosa watu ambao walimpenda na walikuwa tayari kumuoa binti huyu.


Mwanzoni alikuwa akikataa lakini kadiri alivyoendelea kuishi na kuzoea mazingira alisahau kabisa ushauri wa mama na baba yake aliopewa usiku anaposafiri. Ghafla nafsi ilimsukuma kutaka mapenzi na mpenzi wake alimpenda sana Edison na hapo hapo ujauzito akapata.

Walimu waligundua kuwa Anna alikuwa na ujauzito na hivyo alifukuzwa chuoni na ili mbadi srudi Tanzania kwao hakika "ASIYESIKIA LA MKUU HUVUNJIKA GUU"

Kielelezo 9.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali la 9*

Hata hivyo, watahiniwa wengine (33.9%) walishindwa kujibu swali hili na kupata alama za chini, yaani 0 hadi 4. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya uandishi wa insha za kisanaa. Baadhi yao waliandika insha zisizozingatia kichwa cha habari "MAONYO YA WAZAZI" au "WATOTO WASIKILIZENI WAZAZI WENU". Pia, hawakutumia lugha ya kisanaa na wengine waliandika bila kuzingatia muundo rasmi wa insha. Aidha, katika kiini walishindwa kuelezea tabia zisizokubalika katika jamii na badala yake walielezea mambo kadhaa yasiyohusiana na kichwa cha insha walichopewa. Mambo hayo ni kama vile *matawi ya sanaa*, *aina za fasihi* na *mengineyo* kinyume na matakwa ya swali. Pia, hawakutoa hitimisho lenye kuishia na methali "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu" kama

yalivyokuwa matakwa ya swali hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo 9.3 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata 0.


SANAA

Sanaa ni maonesho ambayo huoneshwa sehemu
mbalimbali kuna aina tatu za sanaa kuna sanaa
a ya maigizo kuna sanaa ya maonesho na ku
na sanaa ya uchongaji na sanaa ya uchoraji
tukiangalia sisi watoto tuna kuta tuna pendasa
naa aina nyingi kwa mfano tuki angalia sanaa
ya uchoraji.

Uchoraji. Una kuta mtu anajua kuchora pia
ni mchoraji mzuri ikifika siku ya maonyesho watu
wana kuwa wana enda kuangalia kipaji ulicho
nacho kama uchoraji ana kutua ana kupenda sasa
una kuwa mteja wako wa mambo ya uchoraji
utakuta ana sema naomba unichoree picha nzuri
alafu nita kuja kuchukua una kuwa mejitangaza
zia tayari kipaji chako.

Uchongaji. Uchongaji pia una kuwa ume
jifunza kuchonga vitu mbali mbali kwa aina ya ucho
ngaji una kuwa unajua pia una kuwa una jita
ngaza kipaji mtu ata penda picha uliyo chora atai
penda na ku weza kumnunua.

Uchekeshaji. Nayo ni sanaa ambayo watoto
tuna kuwa tuna penda mambo ya kuchekeshana
kuigiza ili kuwa furahisha watu katika sanaa


Kielelezo 9.3: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali la 9*

Kielelezo 9.3 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika kichwa cha insha, “SANAA” na katika kiini alitoa hoja zinazoelezea *matawi ya sanaa* kinyume na matakwa ya swali.

### 2.3.2 Swali la 10: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Ushairi*) na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza jinsi taswira zilivyotumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe kwa jamii kwa kutoa hoja kutoka katika diwani mbili teule na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa la kuchagua ambapo watahiniwa 230,564 sawa na asilimia 54.3 walilijibu. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo asilimia 78.3 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




Chati Na. 10: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 10. Watahiniwa 103,524 (44.9%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15; watahiniwa 77,008 (33.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 50,032 (21.7%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4.

Asilimia 44.9 ya watahiniwa waliopata alama za juu (10 hadi 15) waliweza kueleza taswira tatu zilizowasilishwa na mwandishi kwa kila diwani na jinsi zilivyowasilisha ujumbe kwa jamii. Watahiniwa hao walikuwa na uwezo wa kutambua taswira mbalimbali zilizojengwa katika diwani teule, kwa hiyo waliweza kuonesha taswira zinazowasilishwa na waandishi katika diwani ya "Wasakatonge", "Malenga Wapya" na "Mashairi ya Chekacheka" na jinsi zilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

Kwa mfano, katika diwani ya "Malenga Wapya" waliweza kuonesha taswira ya "njiwa" ikiwa imetumika kuelezea namna mpenzi wake alivyomuacha na namna anavyohangaika kumtafuta mwingine mwenye sifa nzuri kama huyo. Waliweza pia kubaini taswira ya "mvuvi wa samaki", ikimaanisha tabaka tawala na tabaka tawaliwa (wanyonge) wanavyonyimwa haki zao, hivyo kutakiwa kujikwamua. Taswira nyingine walizobaini katika diwani hii ni pamoja na "ua" ikiwa na maana ya mwanamke au msichana; "Paka shume" akimaanisha wanaume wanaosaliti ndoa zao kwa kuwa na wanawake wengine na; "Punda" ikimaanisha tabaka la chini linalonyonywa na kugandamizwa kwa kukosa haki zao. Katika diwani ya "Wasakatonge" watahiniwa hao walionesha taswira kama “nahodha” na “jahazi” ikiwakilisha *kiongozi* na *nchi*. Msanii ametumia taswira hizi akihusisha na jamii yetu ambayo kuna baadhi ya viongozi ambao wanang’ang’ania madaraka (Nahodha) bila kujali nchi (Jahazi) inaelekea pabaya kwa sababu ya kushindwa kuwajibika ipasavyo. Vile vile, katika diwani ya "Mashairi ya Chekacheka" watahiniwa hao waliweza kuonesha taswira ya "nyati" wakiwa na maana ya mtu kutokuwa mlegevu na muoga kwa kusimamia misingi madhubuti na kutotetereka kwa namna yoyote na "chatu" ikiwa na maana ya wanyonyaji wa mali ya umma. Kwa jumla, watahiniwa hao waliweza kutaja mashairi husika na kunukuu baadhi ya beti za mashairi hayo ili kushadidia kile kilichoelezwa. Kielelezo 10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

10. Taswira; Ni picha inayojengeka akilini mwa msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi. Taswira yaweza kuwa hisi au yaoni Hivyo wasanii wa kazi za fasihi hutumia taswira katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Hii inathibitika kwa kutumia diwani ya "Malenga Wapya" ya TAKILUKI na "Wasakatonge" ya Mohamed S. Khatibu. kuwa wasanii hufikisha ujumbe kwa kutumia taswira;

Tukianza na diwani ya "Malenga Wapya" msanii ametumia taswira ya Paka shume katika shairi la "Kwa nini" kuonyesha wanaume wanaopenda kuchukuwa wanawake wengine hali ya kuwa wana-wake zao. Msanii hapa ametoa onyo kuwa wanaume wanaopenda tabia ya kuchukuwa wanawake wa watu hali ya kuwa nao wana wake zao, waache tabia hiyo kwani huonyesha usaliti. Msanii amesema:

"Wanaume, mwafanyani, nauliza
Pakashume jigeuza,
Ni kwanini."

Pia ametumia taswira ya mshumaa; Katika shairi la "Hali halisi" kuonyesha kuwa Katika nchi yetu tumeshapata uhuru lakini bado tumeshindwa kujiletea maendeleo. Hivyo ametoa ujumbe wa kuwa Viongozi waelewe kuwa lengo la kupata uhuru ni kujikomboa na si kuzidisha matatizo. Hivyo waongoze nchi vizuri. Msanii anauliza,

"Mshumaa unawaka, giza mbona linazidi".

Vilevile msanii ametumia taswira ya

10. "Njiwa" Katika shairi la "Nipate wapi mwingine" Msanii ametumia taswira hii kuonyesha mwanamke aliyekuwa akimtii mumewe, na ametariki, hivyo mume analalamika. Msanii ametumia taswira hii kuwashauri watu ili wafanye mambo mema ili wakifariki waweze kukumbukwa. Msanii anasema,

"Njiwa ameshanitoka, nipate wapi mwingine"

Vilevile katika diwani ya Wasakatonge mwandishi ametumia taswira ya nahodha katika shairi la "Nahodha" akimaanisha kuwa nahodha ni kiongozi, ila kuna baadhi ya watu wanashika nafasi ya unahodha hali ya kuwa hawawezi kuongoza hatimae anawatesa abiria. Hapa msanii ametoa ujumbe wa viongozi wanaopenda kung'ang'ania madaraka hali ya kuwa hawawezi kuongoza waache, kwani wanawatesa ~~vio~~ wananchi. Kama alivyosema katika shairi hilo:

"Nahodha wang'ang'ania usukani
Abiria sote twateseka..".

Si hivyo tu pia ameonyesha taswira ya Jiwe na mchi katika shairi la "Jiwe si mchi" kuonyesha wanawake wanao waocha wanaume na kufanya vitendo vichafu vya kusagana. Hapa ameonyesha ujumbe wa kuwa wanawake wanaoendekeza tabia ya kusagana waache kwani ni kinyume na mila na desturi zetu. Msanii amesema

"Ndafaka haziwi unga, kwa kusagiwa na jiwe,
Utaambulia chenga, mapishi yakuumbue"
"Michi imejaa tele, - - . . .

Kielelezo 10.1: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la 10*

Aidha, asilimia 33.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza

katika kuelezea jinsi taswira zilivyotumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe kwa jamii kupitia diwani teule. Baadhi ya watahiniwa walibaini taswira kwa usahihi lakini walishindwa kufafanua baadhi ya taswira hizo zilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Wasakatonge" alitoa taswira ya “vinyonga” yenye kuonesha viongozi wasaliti. Hata hivyo, alishindwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza kuonesha namna taswira hiyo inavyowasilisha ujumbe kwa jamii. Watahiniwa wengine waliweza kubaini taswira katika diwani husika lakini walishindwa kutaja na kunukuu sehemu ya shairi na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (21.7%) walishindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu 0 hadi 4. Watahiniwa hao walikosa uelewa wa taswira tatu zilizotumiwa na waandishi kwa kila diwani na jinsi zilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii katika diwani teule. Baadhi ya watahiniwa walionesha kutoelewa maana ya taswira kwa kuelezea kuwa ni *maneno yanayogusa hisi*a (kihisishi) badala ya kufafanua taswira kama mbinu ya *kuunda picha ya jambo katika mawazo ya msomaji*. Katika kiini cha swali watahiniwa hao walishindwa kabisa kuonesha taswira zilizotumiwa na waandishi na namna zinavyofikisha ujumbe kwa jamii. Badala yake, walifafanua dhamira zilizojitokeza katika diwani husika. Aidha, watahiniwa wengine walichanganya mashairi ya diwani moja na nyingine, hivyo walielezea taswira zisizo sahihi katika diwani husika na kupata alama hafifu. Kielelezo 10.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.

| | |
|---|---|
| 10. | Taswira; Haya ni mawazo anayokuja nayo |
| | mwandishi kwa lengo la kuelimisha jamii mfano |
| | wa taswira ni kama umaskini, ukosefu wa ajira. |
| | Kwa kutumia diwani mbili ambazo ni za |
| | Mashairi ya chekacheka yaliyo andikwa na T.A mvungi |
| | pamoja na Wasakatonge waandishi wameweza kutu- |
| | mia taswira hizo kuwasilisha ujumbe kwa jamii |
| | kwa kuanza na mashairi ya chekacheka. |
| | Suala la rushwa katika jamii; Mwandishi |
| | wa diwani hii ameweza kuonyesha ni kwa jinsi |
| | gani rushwa inavyoweza kushusha maendeleo ya |
| | jamii na kuwanyonya watu wengine na ametumi |
| | a taswira hii kufikisha ujumbe kwa hadhira |
| | kwamba rushwa ni chanzo cha maendeleo mabo- |
| | ya katika jamii yetu. |
| | Suala la uzembe na ukasuku; Mwandishi |
| | ameweza kuonyesha ni kwa jinsi gani uzembe |
| | unaweza kuleta madhara katika jamii zetu |
| | kama kuchangia kuporomoka kwa maendeleo |

ya inchi yetu. kwahiyo ujumbu aliokuja nao
10 mwandishi ni kwamba tufanye kazi kwa
bidii ili kuepukana na umasikini.

Suala la mapenzi; Pia mwadishi wa
diwani ameweza kuonyesha ni kwa jinsi gani
watu katika jamii waliuyo na mapenzi
yasiyokua ya kweli na ujumbe tunaweza
kupata katika taswira hii ni kwamba
tuonyeshane mapenzi yaliyokua ya kweli baina
yetu.

Pia kwa kutumia diwani ya pili ya
Wasakatonge mwandishi M.S. Khatibu pia amew-
eza kuonyesha baadhi ya taswira ambazo
msanii ameweza kuwasilisha ujumbe kwa jamii
kwa kutumia taswira hizo kama ifuatavyo.

Suala la matabaka Katika jamii; Pia katika
diwani hii mwandishi ameweza kuonyesha
matabaka baina ya walio kua nacho na
wasio nacho na ujumbe utunaoupata katika
diwani hii ni kwamba matabaka katika
jamii zetu yanapelekea ubaguzi baina yetu.

Suala la uongozi mbaya; Hali hii
inajumuisha wale wanaotumia ~~fee~~ madaraka
yao kwa njia zisizofaa ambazo zinaweza kushu-
sha na kudidimiza maendeleo ya jamii na
ujumbe tunao upata ni kwamba tunatakiwa
kuongoza kwa haki ili kujenga nchi yenye
amani.


Siasa; Pia mwandishi wa diwani hii
ameweza kuonyesha suala la siasa liliuyaweza
kuleta madhara katika jamii kama haita
tumika vizuri.

Kielelezo 10.3: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali la 10*

### 2.3.3 Swali la 11: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Riwaya*) na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli kuwa, "Waandishi wa kazi za fasihi huibua migogoro mbalimbali na kupendekeza masuluhisho ili kuelimisha jamii husika" kwa kutoa hoja kutoka katika riwaya mbili teule. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Hili lilikuwa swali la kuchagua ambapo watahiniwa 370,417 sawa na asilimia 87.2 walilijibu. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri ambapo asilimia 86.3 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




Chati Na. 11: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 11*


Chati Na. 11 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11. Watahiniwa 196,691 (53.1%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15; watahiniwa 122,979 (33.2%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 50,747 (13.7%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi ambapo zaidi ya nusu (53.1%) walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kuanzia 10 hadi 15 kwa kuwa waliweza kuthibitisha kauli kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu katika riwaya mbili teule. Watahiniwa hao waliweza kuonesha migogoro na masuluhisho yaliyopendekezwa na waandishi na namna ilivyoelimisha jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia riwaya ya "Takadini" na kueleza mgogoro kati ya Shingai na wazazi wake, chanzo kikiwa Shingai kutaka kuolewa na mtu mwenye ulemavu wa ngozi (Takadini). Suluhisho lake ni ndoa kati ya Shingai na Takadini ambapo jamii inaaswa kuwa suala la ndoa waachiwe wapendanao. Vivyo hivyo, watahiniwa hao waliweza kubainisha migogoro anuai katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" na "Joka la Mdimu" na kuonesha masuluhisho yaliyopendekezwa na waandishi ili kuelimisha jamii husika. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi na kupata alama za juu.

11\. Migogoro ni hali ya kutoelewana baina ya pande mbili. Migogoro huweza kuwa na vyanzo mbalimbali. Waandishi wa kazi za fasihi ni wahandisi wazuri wa kuibua migogoro mbalimbali kisha kutolea masuluhisho. Ili kufikisha ujumbe ambao mtunzi wa kazi ya fasihi amedhamiria ni lazima kuzingatia migogoro iliyosukwa katika kazi ya fasihi. Kauli ya kuwa waandishi wa kazi za fasihi huibua migogoro mbalimbali na kupendekeza masuluhisho imedhibitishwa na waandishi wa riwaya. Ben J. Hanson katika TAKADINI na E. Mbogo katika WATOTO WA MAMA NTILIE wamedhibitisha hilo. Migogoro katika Takadini ni kama ifuatavyo.

Mgogoro kati ya Shingai na familia yake. Mgogoro huu unatokana na kuwa familia ya Shingai imemwandalia mme Shingai aitwaye Nhamo, lakini Shingai anampenda sana Takadini ambaye ni sope. Kitendo cha Shingai kwenda kinyume na familia kunazua mgogoro. Suluhisho la mgogoro ni kuwa Shingai anaamua kukimbilia kwa Takadini, mvulana aliyempenda sana. Mwandishi ametumia mgogoro huu kufasa jamii kuwa suala la ndoa ni la mtu binafsi na wala si familia.

| | |
|---|---|
| 11 | Mgogoro kati ya mzee Makwati na sekai. Mgogoro huu unatokea mara tu baada ya sekai kujifungua mtoto ambaye ni sope. Mzee makwati anakubaliana na mila na desturi kuwa Takadini anapaswa auawe kwa kuwa ni laana katika jamii. Hali ya kuuawa kwa Takadini haikubaliki machoni pa sekai. Suluhisho la mgogoro huu ni sekai kuamua kukimbia na mtoto wake kuelekea kijiji cha mbali hadi Takadi alipooa na kupata mtoto ambaye si sope ndio wakarudi. Mwandishi anasuka mgogoro huu ili kuonya jamii juu ya mila potofu za kuua walemavu wa ngozi (sope). |
| | Mgogoro katika nafsi kwa Tendai. Huu ni mgogoro wa nafsi. Tendai ambaye ni mke wa mwisho wa mtemi masasa anakumbwa na mgogoro wa nafsi. mgogoro huu unatokana na kuolewa na mtemi masasa ambaye ni mkubwa hivyo kutamani kumuita baba. Hali hii inapelekea Tendai kuingia katika mgogoro wa nafsi, Suluhisho la mgogoro huu ni kumtafuta rafiki ambaye ni sekai ili waweze kushirikiana. Mwandishi anatongenzza mgogoro huu wa nafsi ili kuelimisha jamii juu ya suala la ndoa. Kila mtu ana haki ya kupenda anayemtaka. katika riwaya ya WAFOTO WA MAMANTILIE. migogoro ifuatayo imeonekana. |
| | Mgogoro kati ya Dotto na Peter. Mgogoro huu umesukwa maeneo ya jaani ambako peter alienda kuokota mabaki ya vyakula. Mgogoro huu unasababishwa na peter kuingilia eneo ambalo Dotto na kurwa huokota mabaki yao, Mgogoro huu unapelekea hadi watu kugombana. Suluhisho la mgogoro ni Kurwa kumwambia amwache Peter. Mwandishi anasuka mgogoro huu ili kuonesha jamii matatizo yayowakumba watoto wadogo walioghubikwa na wingu la Umaskini. |


11 Mgogoro kati ya zita na Kurwa. Huu ni mgogoro mwingine unaojitokeza baina ya mabinti hawa wawili. Mgogoro huu unatokana na Peter kumleta Kurwa nyumbani ilihali zita hamjui. Hali hii inaleta sintofahamu baina ya watu hawa. Kurwa anatishiwa kupigwa lakini mgogoro unasuluhishwa na Peter kwa kumtuliza na kumweleza iliyokuwa hadi akaja na Kurwa. Mgogoro huu unasukwa ili kuonesha jinsi ambavyo maisha bila malezi ya wazazi yanavyokuwa, watoto wanaishi kwa kurandaranda.

Mgogoro wa nafsi wa Kurwa. Kurwa anaonekana kuwa na mgogoro wa nafsi ndani yake, hii inatokana na kuona watoto wawili wakipita na mama yao huku wakihoji kama wangenunuliwa nguo za sikukuu. Hali hii inampa mawazo Kurwa na kutamani kama angekuwa na wazazi kama wale watoto. Mgogoro huu unaonesha jamii kuwa watoto wa mtaani hutamani kuishi maisha mazuri. Jamii hainabudi kuwaangalia kwa jicho la pili kwa sababu wasiposaidiwa watajiingiza katika vitendo viovu kama vile wizi.

Kwa kumalizia, Migogoro ni msingi wa dhamira na ujumbe kwa sababu migogoro huakisi kilo kinachotokea kwenye jamii, Ufundi wa kusuka migogoro wa waandishi wa vitabu tajwa hapo juu wamesaidia kufikisha ujumbo kwa urahisi katika jamii. Huyo ni dhahiri kuwa waandishi wa kazi za fasihi hulbua migogoro mbalimbali na kupendekeza masuluhisho ili kuelimisha jamii husika.

Kielelezo 11.1: *Sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika katika Swali la 11*

Aidha, asilimia 33.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja sahihi na zisizojitosheleza. Watahiniwa hao waliweza kubainisha migogoro mbalimbali kutoka katika riwaya teule lakini baadhi yao walishindwa kuonesha masuluhisho yaliyopendekezwa na waandishi na wengine hawakuonesha namna inavyoelimisha jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia riwaya ya "Takadini" na

kufafanua migogoro kati ya *Shingai* na *wazazi* wake. Chanzo cha mgogoro huu ni wazazi wa Shingai kukataa binti yao kuolewa na Takadini (sope) jambo ambalo Shingai hakukubaliana nalo na kuamua kutoroka kwenda kwa Takadini. Hata hivyo, mtahiniwa huyo hakuonesha jinsi mgogoro huo ulivyoelimisha jamii kuwa walemavu wanastahili kupewa haki wanazopewa watu wengine katika jamii kama kuoa/kuolewa na anayempenda na si vizuri kuwanyanyapaa watu wenye ulemavu. Vile vile, mtahiniwa mwingine katika riwaya, "Watoto wa Mama N'tilie" alieleza mgogoro uliojitokeza kati ya *Zita* na *Kulwa, Mwalimu Mkuu* na *Wazazi* na kutoa masuluhisho ya migogoro hiyo bila kuonesha namna ilivyoelimisha jamii, hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 11.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza katika swali hili.

11. Waandishi wa kazi ya fasihi huibua migogoro mbalimbali
na kupendekeza masuluhisho ili kuelimisha jamii husika.
Migogoro ni kutokuelewa kwa watu walili au zaidi
au pia nafsi ya mtu na mtu mwenyewe. Waandishi wa
kazi za fasihi huibua migogoro iliyopo katika jamii fulani
na kisha kuzimaliza kwa kupendekeza masuluhisho ili
kuelimisha jamii husika. Kwa kutumia riwaya mbili
nilizosoma "TAKADINI" kilichoandikwa na Ben. Hanson na
WATOTO WA MAMANTILIE" kilichoandikwa na E. Mbogo. kwa
kuanza na kitabu cha Takadini Migogoro ilikuwa;
Mgogoro kati ya Takadini na Nhamo mgogoro huu uli
sababishwa na Shingai kwani Nhamo alikuwa akimpenda Shingai
ila Shingai ~~hamp~~ hakumpenda yeye alimpenda Takadini ila
mgogoro huu ulitatuliwa na shingai kumwambia ukweli Nha
mo kuwa hakuwa akimpenda na alimpenda Takadini kisha
kwenda kuishi nae.
Mgogoro kati ya sekai na wake wenzake huu uli
sababishwa na wivu kati yao kwani Sekai alikuwa aki
pendwa sana na Mumewe na kufanya awe anagombana
na wake wenzake. Mgogoro huu ulitatuliwa baada ya sekai
kubeba mimba pia baada ya yeye kutoroka kijijini.
Mgogoro kati ya shingai na wazazi wake huu
ulisababishwa na wazazi wa shingai kutaka binti yao aolewe na
Nhamo wakati mtoto wao hakumpenda na kumfanya atoroke kwao
kwenda kwa Takadini. Mgogoro huu ulitatuliwa baada ya
Shingai kuzaa mtoto asiyesope ambapo kulileta tasuira mpya
kwa kijiji kizima.
Pia kwa kutumia kitabu cha watoto wa Mamantilie.
Mgogoro kati ya Pita na kurwa huu ulisababishwa na
duki binafsi iliyowafanya wao wagombane na kupigano ila
Mgogoro huu ulimalizwa na ~~p~~ Pita na baadae kuwa marafiki
na kuamua kuishi pamoja kama watoto wa baba mmoja.

Kielelezo 11.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani katika Swali la 11*

Kielelezo 11.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha kwa usahihi baadhi ya migogoro, masuluhisho na kushindwa kuonesha namna migogoro hiyo ilivyoelimisha jamii na kupata alama za wastani.

Licha ya swali hili kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, watahiniwa wachache (50,747) sawa na asilimia 13.7 walifaulu kwa kiwango hafifu kutokana na kukosa maarifa ya kutosha katika kuthibitisha kauli waliyopewa. Baadhi ya watahiniwa walipata alama za chini kwa kushindwa kubainisha migogoro iliyojitokeza, masuluhisho yake na namna mwandishi alivyoelimisha jamii. Watahiniwa wengine walibainisha migogoro katika *tamthiliya* teule kutokana na kukosa uelewa wa riwaya teule walizopewa. Aidha, wapo watahiniwa waliobainisha dhamira mbalimbali katika riwaya teule kinyume na matakwa ya swali na kupata 0. Kielelezo 11.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

11 Migogoro; ni malumbano na shida zilizomo katika jamii fulani. Waandishi wa kazi za fasihi huibua migogoro mbalimbali na kupendekeza masuluhisho ili kuelimisha jamii husika. Kwa kutumia riwaya mbili ambazo ni "TAKADINI" kilichoandikwa na Ben J. Hanson na riwaya ya "WATOTO WA MAMA NTILIE" kilichoandikwa na E. Mbogo inathibitisha kauli hii.


Kwa kutumia riwaya ya "TAKADINI" mwandishi ameibua migogoro mbalimbali na kupendekeza masuluhisho ili kuelimisha jamii

Ubaguzi wa rangi; katika riwaya hii mwandishi amemtumia au amewatumia wanakijiji wa mzee makwati kutowakubali watu wenye ulemavu wa ngozi kwani wanaamini kuwa kuwepo kwao ni laana kwa jamii. Sekai aliyekuwa mama wa Takadini amesuluhisha hilo kupitia Shingai aliyeolewa na Takadini na kuzaa mtoto asiye kuwa na ulemavu wa ngozi.

Imani potofu; katika riwaya watu wa kijiji cha mzee makwati walikuwa na imani potofu juu ya watu wenye ulemavu wa ngozi na kudai wauliwe kwani ni laana kwa jamii. Watu wa makwati walielimika kupitia Takadini aliyezaa mtoto na Shingai asiye kuwa na ulemavu wa ngozi

Ndoa za mitara; katika riwaya hii, Mzee makwati alikuwa na wake zaidi ya mmoja. ambapo ilipelekea kunyanyaswa Sekai kabla ya kuzaa mtoto. Alikuwa akidharauliwa kwani alionekana kama tasa. Kutokata kwake Sekai kulimpelekea kupata mtoto. Kutokata kwake tamaa na kumcha kwake Mungu kulimpatia mtoto.

Katika riwaya ya "~~MAMA~~" "WATOTO WA MAMA NTILIE" mwandishi ameibua migogoro mbalimbali na kupendekeza masuluhisho ili kuelimisha jamii.



Ukosefu wa elimu; katika riwaya hii ya watoto wa mama n'tilie. Mama N'tilie hakuwa na elimu ya madhara ya watoto wake kujiingiza katika kazi wakiwa na umri mdogo ambako ilimpelekea peter kufungwa na zita kufariki kutoka na kung'watwa na mbwa bila kupelekwa hospitali hii imetokana ukosefu wa elimu juu ya hatari ya kuumwa na wanyama.

Umaskini; katika riwaya hii familia ya mama N'tilie ilikuwa ni familia maskini sana. Hivyo ilicowalazimu peter na zita kwenda kuokota vyakula jaani ili waweza kula. Kuokota kwao vyakula ingewasababishia kupata na maradhi mbalimbali kutokana na mazao yapatikanayo jaani. Hata hivyo kwenda kwao jaani na peter kuokota kwake kileci kilimpelekea baba yake kupoteza maisha kutokana na kuisha kwake muda wa matumizi.

Malezi ya mtu mmoja; katika riwaya hii, mama n'tilie peke yake ndiye aliyekuwa akihusika na malezi katika familia yake ambapo ilipelekea kwa watoto wake kumsaidia ili waweze kupata hela ya kwenda shule. kama mzee lomolomo angekuwa akiwajibika katika malezi zita asingepoteza maisha na peter asingeingia kwenye biashara ya madawa ya kulevya

Hivyo basi; waandishi hutunga riwaya mbalimbali ili kuibua migogoro ipatikanayo ndani ya jamiiyo zetu ili kutuwezesha kutambua madhara ya mawazo yatolewayo na mwandishi wa kazi ya fasihi.


Kielelezo 11.3: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu Swali la 11*

Kielelezo 11.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua dhamira zilizojitokeza katika riwaya ya "Watoto wa Mama N’tilie" na "Takadini" kinyume na matakwa ya swali badala ya kuonesha migogoro, masuluhisho yake na namna inavyoelimisha jamii, hivyo kupata alama hafifu.

### 2.3.4 Swali la 12: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Tamthiliya*) na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua madhara yanayotokana na kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana kwa kutoa hoja kutoka katika tamthiliya mbili teule na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilikuwa la kuchagua ambapo watahiniwa 378,075 sawa na asilimia 89.0 walijibu swali hili. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri sana ambapo, asilimia 88.1 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 12:** *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia katika Swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 12. Watahiniwa 168,243 (44.5%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15; watahiniwa 164,841 (43,6%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 44,991 (11.9%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 4.

Watahiniwa 168,243 (44.5%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu 10 hadi 15 kutokana na kufafanua kwa usahihi madhara yanayotokana na kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu "elimu ya jinsia" ambayo ni *maarifa wanayopewa watoto/vijana kwa lengo la kuwafanya kujitambua juu ya mabadiliko ya kimwili na mazingira ili waweze kukabiliana nayo*. Aidha, watahiniwa hao waliweza kuonesha madhara ya kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana katika tamthiliya ya "Orodha", "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" na "Kilio Chetu". Kwa mfano, katika tamthiliya ya "Orodha", waliweza kubainisha madhara, kama vile *maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, ulevi wa pombe, vifo, kujiingiza katika mapenzi bila kujali umri* na *kupata mimba zisizotarajiwa*. Katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" walifafanua madhara ya kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana, kama vile *kuwa wazembe na kukosa uadilifu mahali pa kazi*, *kusababishia serikali hasara kutokana na utendaji mbovu* (kuchanganya kazi na mapenzi) *na kukosa msimamo katika maisha kwa jumla*. Kielelezo 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

12. Elimu ya kijinsia kwa vijana ni elimu ambayo humfanya kijana kuweza kufanya mambo mema na kujitambua yeye kama kijana ili ajiandae kwa ajili ya maisha yanayo fuata baadae hivyo, elimu hii ni muhimu kwa kila kijana.


Madhara yanayotokana na kukosekana kwa elimu ya kijinsia kwa vijana ni kama ifuatavyo, ~~kuto~~ kutokana na Tamthilia ya Kilio chetu na Ngoswe Penzi kitovu cha uzembe.

Yafuatayo ni madhara ya kukosekana kwa elimu ya kijinsia katika tamthilia ya Kilio chetu:-

Mimba za utotoni; Mwandishi wa tamthilia hii ameonyesha kuwa swala la mimba za utotoni lina sababishwa na ukosefu wa elimu ya kijinsia kwa kupitia mhusika Suzi ambaye aliweza kupata mimba akiwa katika umri mdogo kwa sababu mama yake aliona si vyema mtoto wake Suzi kupata elimu ya kijinsia katika umri aliyo kuwa nao.

Maambukizi ya virusi vya Ukimwi; Katika tamthilia hii mwandishi ameonyesha pia kwamba swala la maambukizi ya virusi vya ukimwi yameweza kusababishwa na ukosefu wa elimu ya kijinsia ambayo alitakiwa kupewa kijana Joti kabla ya kupata maambukizi hayo na hivyo elimu ya kijinsia ingetolewa kwa kijana huyo inge saidia kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa wa virusi vya ukimwi.

Kifo; Kifo kilichosababisha kilio cha watu kama Suzi kilisababishwa na ukosefu wa elimu ya kijinsia ambayo ilikosekana kwa kijana Joti hivyo katika tamthilia hii



12. kijana Joti aliweza kupoteza maisha kwa kukosa elimu ya kijinsia ambayo ingeweza kumsaidia katika anga tililo mkumba.

Kwa kutumia tamthilia ya Ngoswe Penzi kitovu cha uzembe ukosefu wa elimu umejadiliwa kuleta madhara kama ifuatavyo:-

Uzembe; katika tamthilia hii ni wazi kuwa Ngoswe alikosa elimu ya kijinsia iliyomfanya hata akawa mzembe na kusahau kazi iliyompeleka katika kijiji cha Mzee Ngengemkeni Mitomingi ambayo ilipelekea uharibifu mkubwa wa kazi ya takwimu za watu na makazi ambapo uharibifu huo ulifanywa na Mzee Ngengemkeni Mitomingi mbele ya Ngoswe kwa kosa la Ngoswe kumtorosha Mazoea binti wa mzee Ngengemke Mitomingi.

Kijana kukosa msimamo; Mazoea amesemekana kama kijana asiye na msimamo katika tamthilia hii kutokana na kukosekana kwa elimu ya kijinsia kwa sababu wakati Ngoswe anamtaka kimahusiano ilihali anajua kuwa ana mtu kwa ajili yake alishindwa kukataa na akamkubalia Ngoswe hatimaye alishia kupewa adhabu kwa sababu mtu aliye mtegemea hakuwa na uwezo wa kuondoka nae baada ya kazi zake kuharibika.

Mgogoro katika familia; Mwandishi anaonyesha kuwa kijana Mazoea angeweza kupewa elimu ya kijinsia asingesababisha mkwaruzano katika familia yake kwani mama yake aliweza kulaumiwa kwa kitendo cha mtoto wake (Mazoea) kuwa na mahusiano ya kimapenzi na Ngoswe muhesabu watu.

Hivyo tamthilia hizi zinatoa funzo kwa jamii juu ya utoaji wa elimu ya kijinsia kwa vijana ili kuwaepusha vijana na madhara kama vifo, na maambukizi ya magonjwa kama Ukimwi.

Kielelezo 12.1: *Sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa katika Swali la 12*

Kielelezo 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha kwa usahihi madhara yaliyotokana na ukosefu wa

elimu ya jinsia kwa vijana katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" na "Kilio Chetu na kupata alama za juu.

Aidha, watahiniwa asilimia 43.6 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa waliweza kufafanua baadhi ya madhara yanayotokana na kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana kwa kutoa hoja sahihi kwa baadhi ya tamthiliya teule na kushindwa katika tamthiliya nyingine. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja chache na zisizojitosheleza kimaudhui kuhusu madhara ya kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua madhara hayo katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" kwa kuonesha utendaji mbovu wa kazi na uzembe wa Ngoswe ulivyozorotesha maendeleo ya jamii yake. Pia, alielezea mwanamke kutumika kama chombo cha starehe na imani za kishirikina lakini hakuweza kuhusisha na ukosefu wa elimu ya jinsia kwa vijana, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache, (44,991) sawa na asilimia 11.9 walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kubainisha madhara yanayotokana na kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana. Hivyo, hawakuweza kutoa ufafanuzi kulingana na swali lilivyoelekeza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kutoa utangulizi na katika kiini hakuweza kutoa ufafanuzi unaoeleweka kuhusiana na madhara ya kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walishindwa kutaja majina ya tamthiliya husika na wengine walibainisha madhara yasiyo sahihi kwa wahusika wake na wengine walifafanua dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule na kupata alama hafifu. Kielelezo 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua madhara ya kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana.

12. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma, fafanua madhara yanayotokana na kukosekana kwa elimu ya jinsia kwa vijana kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila kitabu.

hoja ya kwanza ni vifo mwandishi anatueleza kuwa madhara yanayo tokea kwa jamii mbalimbali kupitia kwenye kitabu mbalimbali.

hoja ya pili ni umasikini katika jamii utokana na kutokuwa na elimu vijana ujitumia vibaya katika jamii ambazo wina elimu ya kutosha.

hoja ya tatu ulevi hii ina waumiza sana vijana kutokujua madhara ya pombe hutumia kama burudani na kuharibu malengo ya vijana.

hoja ya nne magonjwa yanayo tokana na ukeketaji huambukizana kwa kuwa wanatumia dhana moja kwa watu wengi hivyo husababisha magonjwa.

hoja ya tano imani potofu pia husababisha kuto kuelimika kwa haraka hivyo tunashauliwa kuelekezana kiundani zaidi ili jamii iweze kuamini kuwa inaweze kana kutokuwana dhana potofu.

Kielelezo 12.2: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali la 12*

Kielelezo 12.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetaja madhara bila kuhusisha na utendaji wa wahusika katika tamthiliya teule na kupata alama hafifu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA

Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali 12 ambayo yalitoka katika mada ya *Ufahamu, Matumizi ya Sarufi na Utumizi wa Lugha, Uandishi, Maendeleo ya Kiswahili na Fasihi.*

Uchambuzi wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani katika mada zote zilizotahiniwa. Kiwango kizuri cha kufaulu kilikuwa katika mada nyingi kikijumuisha swali la kuchagua (85.7%) lililohusisha mada za *Aina za maneno, Mjengo wa tungo, Fasihi simulizi, Fasihi kwa ujumla na Ngeli za Nomino* (*mada mchanganyiko*), *Ufahamu na Ufupisho* (81.2%), *Fasihi Simulizi* (80.2%) na *Uandishi* (73.2%). Aidha, mada za *Maendeleo ya Kiswahili* (56.6%) na *Matumizi ya Sarufi na Utumizi wa Lugha* (51.8%) zilikuwa na viwango vya wastani vya kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani huu.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2019 kupitia mada mbalimbali kilikuwa ni kizuri. Wastani wa kufaulu kwa mada zote ni (71.5%) ikiwa na ongezeko la asilimia 4.9 ikilinganishwa kiwango cha wastani cha kufaulu kwa mada kwa mwaka 2018, hali inayodhihirisha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Mtihani wa Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2019 ulizingatia Muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi, yaani *kukumbuka, kuelewa, kutumia, kuchambua, kutathmini na kuunda*. Kiwango cha kufaulu kwa jumla kilikuwa kizuri ambapo asilimia 91.31 ya watahiniwa walifaulu somo hili.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa, kama vile kutofuatwa kwa maelekezo ya swali na uelewa mdogo kwa baadhi ya mada, hususan mada za *Matumizi ya Sarufi/Utumizi wa Lugha* na *Maendeleo ya Kiswahili*. Ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu kwa mada

zote katika mtihani wa Kidato cha Nne, mikakati mbalimbali inahitajika katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mada ya *Matumizi ya Sarufi/Utumizi wa Lugha* na *Maendeleo ya Kiswahili* sharti zitiliwe mkazo zaidi katika mbinu zitumikazo kufundishia mada hizo. Hii ikiwa ni pamoja na walimu kufundisha kwa kutumia mbinu shirikishi na kutoa mazoezi ya kutosha. Walimu wanapaswa pia kuwaongoza wanafunzi katika kufanya utafiti/kazimradi ili kubaini miundo ya maneno mbalimbali ya Kiswahili, matumizi ya lugha ya Kiswahili na uhusiano baina ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Kwa jumla, mbinu hizo zinalenga kuwawezesha watahiniwa kupata ujuzi wa kujieleza kwa ufasaha na kukuza msamiati wa lugha ya Kiswahili, hasa ikizingatiwa kuwa *sarufi* na *matumizi ya lugha* ndiyo msingi wa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

Aidha, kumekuwepo na kupanda na kushuka kwa viwango vya kufaulu kwa baadhi ya mada zilizotahiniwa kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na viwango vya kufaulu vya mwaka 2018. Mada iliyopanda ni *Ufahamu* pekee ambayo ina nyongeza ya asilimia 6.9 kutoka (74.3 %) na kuwa (81.2%). Mada nyingine zote zilishuka ambapo mada ya *Uandishi* imeshuka kwa asilimia 15.4 kutoka (88.6%) na kuwa (73.2%), *Fasihi* (9.3%) kutoka (89.5%) na kuwa (80.2%), *Maendeleo ya Kiswahili* (17.7%) kutoka (74.3%) na kuwa (56.6%) na *Sarufi na Utumizi wa Lugha* (12.3%) kutoka (64.1%) na kuwa (51.8%).

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha watahiniwa cha kufaulu katika somo la Kiswahili. Pia, itasaidia kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hali hii itawafanya walimu na watahiniwa kuyaelewa makosa mbalimbali yanayosababisha kufaulu kwa kiwango cha chini ili kuweza kufanya marekebisho kwa ajili ya kuinua kiwango cha kufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuongeza kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika somo la Kiswahili, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

5.1 Wanafunzi wazoeshwe kufanya utafiti katika lugha zao za asili na lugha ya Kiswahili ili wapate maarifa ya kutosha kuhusu asili za lugha mbalimbali na tofauti zinazoweza kubainishwa katika lugha moja na nyingine.

5.2 Wanafunzi wasisitizwe kutumia sarufi sahihi ya tungo za Kiswahili ili kujijengea weledi katika mada ya *Uundaji wa Maneno/Tungo* ili kuondokana na tatizo la matumizi ya maneno na tungo zisizo sahihi.

5.3 Wanafunzi wahamasishwe kujihusisha na utunzi wa insha za hoja na za kisanaa ili kuinua vipaji vya uandishi wa makala mbalimbali. Aidha, wasisitizwe kushiriki mashindano ya uandishi wa insha kiwilaya, kimkoa na kitaifa.

5.4 Kutiliwe mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa kupewa uzito sawa. Aidha, watahiniwa wahamasishwe kusoma vitabu vya kiada na ziada na kufanya mazoezi mbalimbali yanayohusiana na mada hizo.

5.5 Wanafunzi wahusishwe katika mbinu shirikishi za ujifunzaji na ufundishaji, kama vile majadiliano, onesho mbinu na nyinginezo ili kuwawezesha kuelewa kwa haraka, kuwa wabunifu na kujengewa uwezo wa udadisi.

KIAMBATANISHO A

**UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI**

| **Na.** | **Mada** | **Kufaulu kwa kila Swali** | | **Wastani wa Kufaulu (%)** | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Na. ya Swali** | **% ya Kufaulu (alama $30^{+}$)** | | |
| 1. | *Mada Mchanganyiko* | 1 | 85.7 | 85.7 | Vizuri |
| 2. | *Ufahamu* | 8 | 81.2 | 81.2 | Vizuri |
| 3. | *Fasihi* | 4 | 63.9% | 80.2 | Vizuri |
| | | 7 | 84.4 | | |
| | | 10 | 78.3 | | |
| | | 11 | 86.3 | | |
| | | 12 | 88.1 | | |
| 4. | *Uandishi* | 2 | 80.2.1 | 73.2 | Wastani |
| | | 9 | 66.1 | | |
| 5. | *Maendeleo ya Kiswahili* | 6 | 56.6 | 56.6 | Wastani |
| 6 | *Sarufi* | 3 | 49.9 | 51.8 | Wastani |
| | | 5 | 53.6 | | |